# Ni Nini Kinachovutia Kule Mlimani?

Jeffersonville, Indiana USA

Julai 25, 1964J

1 Amini tu, amini tu,
Mambo yote yanawezekana, amini tu.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

Baba Mungu, hayo ndiyo maombi yetu ya kweli usiku wa leo, tukiona yote unayowatendea watu katika siku hii. Nasi tunakuomba Wewe, Bwana, jalia tuamini tu, tuamini tu kwamba Ni Kweli, Neno lililoandikwa likidhihirishwa kwetu. Tujalie mambo haya, Baba.

Sasa usiku wa leo tunataka kukushukuru kwa ajili ya—ya Nuru uliyotupa kwenye Maandiko kwa ajili yetu asubuhi ya leo. Nasi tunaomba usiku wa leo, Bwana, katika mstari huo wa maombi, ya kwamba utathibitisha Neno Lako kuwa ni Kweli.

Tunayaombea makanisa yote na makusanyiko ambayo yamekusanyika kuzunguka vile—vile—vile vipaza sauti vidogo nchini kote, kutoka kwenye taifa, kote kote hata kwenye Pwani ya Magharibi, kule juu kwenye milima ya Arizona, chini kwenye mabonde ya Texas, mbali sana hata Pwani ya Mashariki, nchini kote, Bwana, ambako wao wamekutanika. Tumeachana kwa masaa mengi, tuko katika wakati, lakini, Bwana, tuko pamoja usiku wa leo kama kundi moja, waaminio, tukingojea Kuja kwa Masihi. Tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utamtuma Yeye hivi karibuni kwa ajili ya Kanisa Lako. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

2 Mnaweza kuketi. Salamu za Kikristo kwa wote walio hapa usiku wa leo. Ninasikitika ya kwamba tungali tumesongamana na tumesheheni hata ni vigumu kupumua. Hata viyoyozi, hata vikifanya kazi vipi, havina nguvu nyingi, watu wengi sana. Kama hakungekuwa na kanisa la kawaida lililojaa watu, hivyo viyoyozi vingewagandisha. Lakini sasa kila mtu ana pepeoi, anajipepea, na kiyoyozi kinavuma kwa nguvu kiwezavyo.

Tunatuma salamu kutoka Pwani ya Mashariki kwenda Magharibi, kwa marafiki wetu wote katika Kristo, wanaosikiliza. Tunatuma salamu kule San Jose, Ndugu Borders, lile kundi kule juu. Tunatuma salamu huko milimani, Prescott, Arizona, kwa Ndugu Leo Mercier na kundi lake walio kule juu wakingojea Kuja kwa Bwana. Tunatuma salamu kwa wale walio Tucson, ambao wamekusanyika usiku wa leo, wakingojea Kuja kwa Bwana. Huko chini Houston, Texas, kwa wale wanaongojea Kuja kwa Bwana. Huko juu Chicago, kwa wale wanaongojea Kuja kwa Bwana. Huko juu kwenye Pwani ya Mashariki, New York na Connecticut, na makundi makubwa kule juu, yanayongojea Kuja kwa Bwana. Hatuna nafasi hapa ya kuwaketisha, kwa hiyo inatubidi tu kuwatumia Neno kupitia—kwa njia ya simu. Tunatuma salamu kwa Ndugu Junior Jackson usiku wa leo, na kundi lake huko Clarksville. Ndugu Ruddell, kule sitini na mbili, na kundi lake, wakingojea Kuja kwa Bwana. Nasi tumekusanyika hapa usiku wa leo kwenye kanisa la nyumbani, yale maskani, tukingojea Kuja kwa Bwana.

3 Na sasa, wengi wenu labda hawakuwa kwenye ibada asubuhi ya leo. Lakini ninatumaini ya kwamba kila mtu, ambaye hakuwako, atapata kanda hiyo, kwa kuwa ninaamini ya kwamba ulikuwa ndio Ujumbe ulio moja kwa moja sana kwa kanisa tangu ule—Ujumbe wa Mabwana, Ni Wakati Gani? Nilihisi upako wa Roho, nikajisikia kuongozwa kusema yale niliyosema. Ulikuwa ni mrefu, lakini hata hivyo nilijisikia kuongozwa kufanya hivyo. Nami nafikiri Bwana, kwa Neno Lake, alionyesha ni saa gani tunayoishi. Na kuhakikisha kwamba tunafahamu mambo haya ya ajabu yanayotendeka. Mwajua, Biblia ilisema, "Wenye hekima watafahamu."

Lakini mataifa na watu watakuwa "wanyonge na werevu zaidi." Hebu fikiria, Mmarekani wa wastani sasa hufikia umri wa kati, yapata miaka ishirini, mnyonge bali mwerevu. Wao hawakuwa na eropleni siku hizo, na—na makombora ya atomiki, bali waliishi miaka mingi zaidi. Tunazidi kuwa wanyonge na werevu zaidi, na hekima yetu wenyewe ndiyo itakayotuangamiza. Tutajiangamiza wenyewe. Mungu hatatuangamiza; hekima yetu itatuangamiza. Daima imekuwa hivyo, na ndivyo itakavyokuwa tena.

4 Sasa, Bwana akipenda, Jumapili ijayo asubuhi, bila kujua sasa yale nitakayohubiri, bali ninatumaini ya kwamba Bwana, kama akituruhusu tuishi na kusitokee cho chote, na ni mapenzi Yake, tunakusudia kuhubiri Ujumbe mwingine Jumapili ijayo asubuhi , kuwaombea wagonjwa Jumapili ijayo usiku. Ndipo inanipasa kurudi nyumbani Arizona, kuirudisha familia ili watoto waweze kujiandikisha shuleni. Ndipo utakuwa … Ndipo nanyi mta…Tutawaarifu, tuwezavyo, juu ya mikutano inapotayarishwa, ama nyakati ambazo tuna…mahali ambapo tunatarajia kuwa. Kwa hiyo, Mungu awabariki nyote.

Sasa usiku wa leo, tukijua ya kwamba ni … Sasa usiku wa leo, tunapojua ya kwamba ni…Kwanza nimechelewa kwa muda wa dakika kumi na tano, saa mbili kasorobo hapa Jeffersonville, na hiyo ni kama saa tatu kasorobo kule—kule Pwani ya Mashariki; na ndipo yapata saa kumi na moja kwenye Pwani ya Magharibi. Kwa hivyo tuko karibu machweo ya jua hapa. Kwa hiyo sasa tuko karibu machweo hapa. Nami nataka kuzungumza nanyi kwa ajili ya ibada fupi tu, kujaribu kupata upako wa Roho, halafu niite mstari wa maombi.

5 Nami ninataka kusanyiko hapa, pamoja na kusanyiko lililokusanyika mahali pengine, kumtafuta mtu fulani, ndugu fulani aliyetiwa mafuta na Roho; na wakati tutakapoanza kuwaombea wagonjwa, aende akawawekelee mikono wale walio kwenye makutano yenu. Kumbuka, Mungu yuko kila mahali; Yeye yuko kila mahali. Kwa hiyo, huko Texas, huko California, huko Arizona, popote ulipo, weka mikono juu ya wale walio wagonjwa tunapoanza kuwaombea wagonjwa. Nami nina hakika Mungu atayasikia na kuyajibu maombi.

Jambo la ajabu, Jumapili iliyopita usiku, na upako ulikuwa ukiendelea, na Roho Mtakatifu … Lilikuwa ni jambo la ajabu. Sikuwa nimekuwa na m—mstari wa utambuzi kwa miezi na miezi, tangu nilipokuwa hapa wakati uliopita. Na halafu kutembea kule chini ya ahadi … Hujui ya kwamba Yeye atatimiza. Huwezi kusema atatimiza. Huna budi kutembea tu pale na kungojea. Yeye ni mwenye mamlaka. Yeye hufanya yale anayotaka. Bali simama pale na kungojea uone atakachofanya, ndipo unasikie ikikujia namna hiyo.

6 Na mwishoni mwa ule—ule mkutano, bila kujua ilikuwa ni nani, bali kulikuwako na m—mtu mahali fulani kwenye mstari aliyekuwa mrefu, na mwenye upara juu, naye alikuwa ni mgonjwa sana.

Na ndipo mwishowe pakatokea mtu fulani hapa jukwaani, naye ameinamisha kichwa chake, naye alionekana mwenye kuugua, ameshika tumbo lake. Nami nikadhani huenda huyo akawa yule mtu wa kwanza ama mtu wa pili, ama po pote ilipokuwepo ambaye nilimwombea, maana alikuwa na upara na ameinamisha kichwa chake; mtu mkubwa, aliyeinama Lakini nilitazama huku na huko nikamkuta yule muungwana ameketi pale, lakini alikuwa akifurahi. Nikawaza, “Iko wapi?” Nisingeweza kuamua ilikuwa wapi. Ningeweza kulihisi na kumwona mtu huyo mbele yangu.

Nikaihisi ikivuta upande huu, nayo ilikuwa ikitoka nyuma. Nilimwangalia Ndugu Neville na hawa wawili walioketi hapa, haikuwa wao. Nikasema, “Mtu huyo yuko upande wa ndani wa kile chumba cha kubatizia nyuma kule.” Nanyi mnajua ilikuwa ni nani? Ndugu Shepherd. Sababu ya mimi kutomtambua, alikuwa ameketi kule nyuma ameinamisha kichwa chake, akiomba.

Alifikiri atakufa, amefikiria jambo hilo kwa majuma machache yaliyopita. Mkewe alimwambia aende akachukue jozi mpya ya viatu, naye akasema, “Sitahitaji. Sitakuwa hapa muda huo wote.”

7 Naye alikutana nami hivi majuzi kwenye…kule uwanjani kwa Ndugu Wood akipaza sauti na kumsifu Mungu. Kasema, “Ninakula nyama ya nguruwe, mayai, nyanya, cho chote ninachotaka.”

Na kwa unyenyekevu akatoa kiti chake, akarudi kule nje kabisa, akiomba. Mnaona, huhitaji kadi ya maombi, unahitaji tu imani. Mnaona?

Sasa, sikujua kama aliponywa ama hakuponywa, nilisema tu, “M—mtu, akiomba, ana kitu fulani hakiko sawa.” Nafikiri alitaja ilikuwa nini, “Tatizo la tumbo, na anaombea nyuma hapa. Bwana Yesu amekuponya.” Sasa, hayo tu ndiyo ningeweza kusema. Mvuto ulikuwa kwamba alikuwa akiomba. Ningeweza kuliona, lakini kinachotendeka sijui. Mnaona?

Bali unapoiona ikirudi, kila mmoja anatambua, Inaposema, “BWANA ASEMA HIVI,” waona, huyo si mimi ninayenena tena, huyo ni Yeye.

8 Lakini daima ninasema, “Yesu Kristo amekuponya,” hiyo ni Kweli kabisa. “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Mnaona? Mnaona?

Lakini linapokuja, “BWANA ASEMA HIVI,” na kukwambia la kufanya na litakalotukia, angalia jambo hilo, itakuwa hivyo.

Lakini ninaposema, “Yesu Kristo hukuponya na hukupa afya,” unaamini, maana Yeye tayari ameshasema hivyo. Ninarudia tu yale aliyosema.

Na ono ni kurudia tu yale aliyoonesha. Mnaelewa?

9 Sasa na tuharakishe na tuingie moja kwa moja kwenye Neno, kwa sababu ninajua ya kwamba wengi wenu mko hapa, mna umbali mrefu wa kusafiri usiku wa leo. Ninaomba ya kwamba Mungu atawabariki, awasaidie na kuwalinda njiani. Na sasa nataka kufungua usiku wa leo katika Mathayo Mtakatifu, sura ya 21, na aya ya 1 hadi 11, katika Mathayo Mtakatifu. Na, sasa, kama huna Biblia yako, ama kama unataka kuandika Maandiko haya, vema.

10 Na sasa kwenu ninyi ambao hamkusikia Ujumbe asubuhi ya leo, nanyi mna kinasa sauti; kamwe hatutaki, kuuza kanda. Kamwe hatupendelei, kuuza kitu chochote. Wakati mwingine katika mkutano mkubwa watatangaza wana vitabu huko nyuma; hatupati faida yo yote kwavyo. Ndugu Vayle ndiye mwandishi. Zile kanda, mtu ambaye hushughulikia kazi ya kanda pale atawaambieni, hatupati pesa kwa kanda. Hatuninii … Si “kanda”; ni Ujumbe. Na wakati mtu anapofikiria kwamba ni pesa, hatatengeneza kanda tena. Hiyo ni kweli. Nilikuwa nikiuliza juu ya jambo hilo, nafikiri kanda zetu zinauzwa yapata, chini ya dola tano, ama kitu fulani, tatu hadi tano, ama kitu kama hicho. Unasema nini? Tatu; na nne, kwa hizo kanda kubwa, ndefu.

Na mhudumu fulani, niliuliza kuhusu moja ya kanda zake, na ilikuwa dola tisa, kama dakika ishirini au thelathini, za ujumbe.

11 Kwa hivyo naona ya kwamba Ndugu yetu Sothmann kule nyuma hatajiriki, ye yote wao, kwa hizi kanda ambazo wana—wanasambaza. Mnaona, wanapata tu za kutosha kuendeleza kazi. Siwezi kuwaomba wazitengeneze bure, kwa sababu hawana budi kununua kanda na kila kitu kingine. Na mitambo hiyo ni ghali sana, inagharimu kama dola elfu kumi kuiweka tayari kutengeneza kanda hizo, kwanza.

Basi, naelewa kwamba hivi karibuni mimi…Wao hawajalitangaza bado. Lakini kuna kusikilizwa kwa kanda tena. Mara kwa mara sisi…wadhamini, mimi sihusiki nayo kamwe. Hata si…sijapata kuwa katika wo wote wa mikutano hiyo. Siko upande huu wala ule. Wao hutuma maombi yao, wadhamini huamua ni nani atakayefuata kwa kutengeneza hizi kanda, nao wanamtumia barua. Hayo tu ndiyo ninayojua juu yake. Wao hushughulikia jambo hilo, kwa sababu hata siwezi kuwaweka wakfu watoto wachilia mbali kushughulikia kanda, kwa hiyo, ama kubatiza.

12 Kwa hivyo moyo wangu wote umo kwenye Ujumbe huu, huo ndio ule Mvuto wa Tatu, na ndio unaonipasa kuwa mwaminifu na mnyenyekevu kwake.

Mathayo 21:1 hadi 11. Nilisema hivyo ili mweze kuwa mkitazamia ninii … ama kuyafungua Maandiko.

*Hata walipo ... karibia Yerusalemu, na kufika Bethfage, katika mlima wa Mizeituni, ... ndipo Yesu alipotuma wanafunzi wawili akiwaambia,*

*Akawaambia, Enendeni mpaka kijiji kile kinachowakabili, na mara mtaona punda amefungwa, na mwana-punda pamoja naye; wafungueni mniletee.*

*Na kama mtu akiwaambia neno, semeni, Bwana anawahitaji; na mara huyo atawapeleka.*

*Haya yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema,*

*Mwambieni binti Sayuni Tazama, mfalme wako anakuja kwako, Mpole, ... naye amepanda punda, Na mwana-punda, mtoto wa punda.*

*Wale wanafunzi wakaenda zao, wakafanya kama Yesu alivyowaamuru,*

*wakamleta yu—yule punda na mwana-punda, wakaweka nguo zao juu yao, naye akaketi juu yake.*

*Watu wengi katika ule mkutano wakatandaza nguo zao njiani; na wengine wakakata matawi ya miti, wakayatandaza njiani.*

*Na makutano waliotangulia, na wale waliofuata, wakapaza sauti, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi; ndiye mbarikiwa, yeye ajaye kwa jina la Bwana; Hosana juu mbinguni.*

*Hata alipoingia Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakisema, Ni nani huyu?*

*Makutano wakasema, Huyu ni yule nabii, Yesu, wa Nazareti ya Galilaya.*

Sasa kama ningechukua somo kutoka kwenye hilo, kwa kama dakika thelathini kabla ya mstari wa maombi kuanza, ningetaka kuchukua hili kwa ajili ya somo: Nini Kinachovutia Kule Mlimani?

13 Sasa, ilikuwa imechosha sana, siku ya wasiwasi, na ilikuwa ni siku isiyo ya kawaida. Tunamwona Yesu hapa akija Yerusalemu, tayari kuhudhuria pasaka. Na pasaka ni pale ambapo mwana -kondoo wa pasaka aliuawa, na damu ikatandazwa juu ya kiti cha rehema kwa ajili ya—upatanisho kwa—kwa ajili ya watu. Naye alikuwa amepanda kutoka Bethfage na alikuwa amekuja kwenye kilele cha Mlima wa Mizeituni, ambao unaangalia chini kwenye kilima kingine kidogo ambapo Yerusalemu ilijengwa. Naye alipokuwa akitazama, alijua ya kwamba huku kulikuwa kuzuru Kwake kwa mwisho.

Huu ulikuwa ndio wakati ambapo Yeye angekabidhiwa mikononi mwa watu wenye dhambi nao wangemwua. Yeye angekufa kifo cha kutisha sana alichopata kufa mwanadamu, na kuzikwa. Yeye angesalitiwa na walio Wake, baadhi yao wakisimama moja kwa moja pamoja Naye. Na Yeye, akiwa Mungu, alijua kilichokuwa mioyoni mwao, na alijua tangu mwanzo ni nani atakayemsaliti. Na alijua ya kwamba mtu huyo alikuwa pamoja Naye ambaye aliketi kando Yake na kumhesabia fedha Zake, na kadhalika, alijua ya kwamba mtu huyo angemsaliti. Na alijua ya kwamba msalaba katili wa Kirumi ulimngojea kule. Alijua ya kwamba maji mwilini Mwake na Damu ya mwili Wake vingetengana, na ya kwamba Damu ingetiririka kutoka paji la uso wake katika matone makubwa kama jasho. Alijua yote yaliyokuwa mbele Zake. Naye anasimama juu ya mlima, akiangalia Yerusalemu.

14 Watu wa siku hizo,…walivyojiita siku hizo “tabaka bora ya watu wa kidini,” walimchukia. Makanisa ya siku hiyo yalimchukia na kumlaumu, na kulaani wote waliomsikiliza. Na kama walienda na kuhudhuria

kampeni Zake, walifukuzwa mara moja kutoka kwenye ushirika wa kanisa. Si ajabu Maandiko yalisema, "Alikuja kwa walio Wake, na walio Wake hawakumpokea." Wale waliopaswa kumpenda, wale waliopaswa kumsaidia, walikuwa maadui Wake, maadui Wake wenye uchungu sana.

15 Naye alikuwa ameunda kundi Lake dogo kutoka kwa kundi la watu maskini, wavuvi, watoza ushuru, wasio na elimu. Biblia ilisema baadhi yao hata walikuwa "wasio na elimu, wasio na maarifa." Wengine hawangeweza hata kuandika majina yao. Yeye kamwe hakwenda makanisani kuwapata watu Wake.

Na kamwe hakukubaliana na yeyote wa viongozi wa kanisa. Na, mbali na hayo, Yeye alifuata mwenendo ule ule wa nabii. Yeye alilaani kila kitu walichofanya, kama walivyofanya wale walio mbele Zake; kwa sababu walikuwa sehemu ya Neno, Naye alikuwa Neno katika utimilifu Wake.

16 Bali katikati ya hayo yote, kupitia kila wakati na kila nabii ambaye alikuwako ama ambaye angekuwako, kutakuweko kiasi fulani cha watu ambao wamechaguliwa tangu asili kusikia Ujumbe huo, nao wataufuata. Hao hawajali umati wa watu. Hawajali lawama za wasioamini. Wao—wao hawabishani nao. Wana wajibu mmoja, huo ni kuamini na kupata kila sehemu Yake wawezayo, walililowesha kama Mariamu aliyeketi miguuni pa Yesu.

Naye Maritha alikuwa akimtengenezea chakula Chake cha njioni, naye Yesu akamwambia, "Lakini Maritha, unashughulikia mambo ya maisha, bali Mariamu ametafuta mambo bora zaidi," mwaona, mambo ya Uzima wa Milele.

17 Sasa, tunaona ya kwamba wengi wa watu waliokuwa wameelewa… Wao hawakuwa na vitabu kama tulivyo navyo siku hizi, hawakuwa na televisheni ama simu, ama cho chote kile siku hizo, bali kulikuwa na fununu ya kwamba Yeye angehudhuria pasaka. Kwa maana wengi wa watu wale, wakiwa watu wa kiroho, walijua ya kwamba Yeye alikuwa yule Mwana-Kondoo wa Pasaka, kwa maana tayari alikuwa amewaambia mambo ambayo yangetendeka.

18 Na halafu, bila shaka, wakijua ya kwamba Yeye angekuwako, na kumpenda namna walivyompenda, walikuwa wakimngojea Yeye. Kulikuwa umati ambao labda ulikuwa ukisukumana, wakibuburushana toka lango hadi lingine, wakiwa macho sana, kwa maana walijua angefika wakati wo wote. Walikuwa wakiangalia.

Wengine walikuwa wakishangaa watu hawa wana nini kukimbia kutoka lango moja kufikia lingine. "Wanavutiwa na nini?"

Nao wangeangalia huku na kuangalia upande ule, wapate kujua. Ilionekana kana kwamba walikuwa wakitafuta jambo fulani, chini ya matarajio ya jambo fulani litakalotukia.

Loo, namna ambavyo ningetaka kubadilisha somo langu kwa dakika chache na kusema jambo hili, kwamba hiyo ndiyo shida leo. Watu ambao wanatazamia kuja Kwake wana hamu sana na matarajio makuu. Tunaweza kuuhisi, ule mkandamizo. Nao wanatafuta, wakiangalia kila mwendo na kila ishara, wakilinganisha na Maandiko.

19 Na wakati walipoona mambo hayo yote yaliyotabiriwa juu Yake, mpaka mwisho, walijua mwisho ulikuwa umekaribia. Walitaka kuwa pale, kwa hiyo wakaangalia. Sehemu ya umati wa watu ilikuwa ni kwa ajili Yake, katika uchache. Wengine walikuwa wakimpinga, wengi wao, asilimia tisini walikuwa wakimpinga.

Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi katika umati wa kidini, wakati inapofikia Neno na Kristo, kuna karibu asilimia moja ambao wangeamini. Ile sehemu nyingine hawagelijali kamwe, hata ifanywe nini, wao wangelifanyia mzaha ama kulikashifu. Vile vile tu. Wakati, mambo hayabadiliki sana, historia hujirudia yenyewe pande zote.

20 Vema, tunaona hiyo ilisababisha wasiwasi. Ilibidi kufanya hivyo. Haina budi kufanya hivyo. Walikuwa wakingojea, walikuwa wakishangaa atafanya nini atakapofika kule. Walitaka kuwa pale wapate lolote angefanya. Walitaka hilo. Walitaka kuliona. Wao walimwamini Yeye. Wengine walikuwa wamesikia Yeye yuaja, nao wakaenda kule kumdhihaki. Kwa hiyo baada ya matarajio yote ya wasiwasi, siku isiyo ya kawaida sana, wakati usiokuwa wa kawaida sana, makanisa yalilala, watu wamejaa wasiwasi, kulikuwako na watu wengi sana pale, na ndipo likatukia!

21 Juu ya Mlima wa Mizeituni kukaja maskini punda mweupe, akishuka chini ya kile kilima, huku kundi la watu likishangilia kwa fujo, wakikata majani ya mitende, wakitupa nguo zao barabarani, wakipiga makelele, "Hosana Mwana wa Daudi ajaye katika Jina la Bwana!" Yule…maskini nyumbu huyu, Mpandaji wake alikuwa si mwingine ila Masihi mpakwa mafuta wa Mungu kwa ajili ya wakati huo.

Mungu, basi, Yeye alikuwa akifanya nini? Ni nini kinachovutia kule juu kilimani? Ni Mungu akifanya historia, na Mungu akitimiza unabii. Na hilo daima husababisha mvuto. Huwakusanya wapinzani wote, wale nderi (wa ujumbe wa asuhuhi hii), na tai pia. Mnaona? Wanakutana wapate kujua kinachoendelea. Wengine wanakuja kwa ajili ya udadisi, wengine wanakuja kutafuta kosa, wengine wanakuja kukosoa.

Watu wa kila aina hukusanyika, kama tulivyosema asubuhi ya leo: waamini, wajifanyao waamini, na wasioamini. Kuna nini mlimani? Unabii unatimizwa. Sasa tutaona kitakachotukia.

22 Sasa, katika Kitabu cha Zekaria, katika mlango wa 9 na kifungu cha 9. Zekaria, mmoja wa manabii, alinena katika Roho, akisema jambo hili.

> *Furahi sana, Ee binti Sayuni; Piga kelele, Ee binti Yerusalemu; Tazama, mfalme wako anakuja kwako; Ni mwenye haki, naye ana wokovu; Ni mnyenyekevu, amepanda punda, Naam, mwana-punda, mtoto wa punda.*

Sasa, hao waandishi walikuwa na shida gani? Hao makuhani walikuwa na shida gani? Watu hao wa dini walikuwa na shida gani? Hili liliandikwa miaka mia nne na themanini na saba kabla halijatukia, na nabii aliyethibitishwa, na tayari liliwekwa katika maandishi na kuitwa Biblia, magombo ya Agano la Kale. Kwa nini hawakuweza kuona ya kwamba huo ni unabii ukitimizwa? Sababu ile ile hawawezi kuliona leo. Walikuwa wamelichukua Neno la Mungu na kulitangua mbele za watu, kwa kufundisha (kwa mapokeo) Mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.

Na kama mwandishi, wahubiri, wahudumu, watu wa kiroho (wanaojiita), watiwa mafuta, wangesoma tu Biblia, wasingekuwa wakishangaa ni kitu gani kinachotendeka, wangejua ni kitu gani. Mungu akitimiza Neno Lake!

23 Historia ilikuwa ikitengenezwa, unabii ulikuwa ukitimizwa. Wokovu kwa ulimwengu ulikuwa ukiwadia, ile siku kuu ambayo manabii wote walikuwa wakiitazamia. Wote waliokuwa kaburini walikuwa wakiingojea siku hiyo (jamani, wazia hilo), wote waliokufa, wote wenye haki kwa damu ya wafia imani na manabii.

Ambapo alikuwa tayari amepaza sauti, "Yerusalemu, Ee Yerusalemu, umuuaye kila nabii ninayemtuma kwako, na kuwaua wenye haki, ni mara ngapi ningekufunika kwa mabawa kama vile kuku kwa vifaranga vyake, lakini hukutaka! Lakini sasa saa yako imefika."

24 Kila kitu kilichokuwa kaburini, Ibrahimu, Isaka, Yakobo, manabii wote, walikuwa wakingojea saa hii.

Nalo kanisa lilikuwa limepofuka Kwayo. "Ni nani huyu anayesababisha kelele hizi zote? Jamaa huyo ni nani?" Walisema wakati mmoja, "Huyo si ni yule mwana wa seremala hapa? Tunamjua. Yeye alipata wapi hekima hii? Mbona, hatumwoni akiunganishwa na shule zetu zozote. Hatujui vitabu vyovyote alivyopata kujifunza kutoka humo. Ni nani Huyo?"

Yeye alikuwa jibu la unabii wa nabii. Huyu hapa anakuja, amepanda mwana punda. Ni mvuto ulioje! Mungu alikuwa akitimiza Neno Lake lililoahidiwa, ile saa iliyokuwa ikisubiriwa tangu miaka elfu nne. Katika Mwanzo, mlango wa 3 na kifungu cha 15, Mungu alikuwa ametabiri, "Uzao wa mwanamke utakiponda kichwa cha nyoka, bali kichwa chake kitakiponda kisigino chake," huo unabii kule kwenye Biblia uliokuwa umebashiri kuja kwa mtu huyu.

25 Na hapa hivi majuzi tu kulikuwako na nabii aliyesimama miongoni mwao, ambaye alithibitishwa kuwa nabii, Zekaria, naye akasema, ya kwamba, "Enyi binti za Yerusalemu na ninyi binti za Sayuni, furahini, piga makelele, paza sauti, kwa maana Mfalme wako anakuja. kwenu, mtiifu, mpole, mnyenyekevu, amepanda mwana-punda."

Na hapa watu wale waliosoma Andiko hilo, siku baada ya siku, walimwangalia akiingia amepanda, na kulia, "Ni nani huyu?" Mnaona? Mungu akilitimiza Neno Lake kwa watu ambao walipaswa kujua lilikuwa ni nini, bali hawakujua.

Mungu anapotimiza Neno Lake, daima huleta mvuto, daima hufanya hivyo. Husababisha mvuto, kwa kuwa Huo si wa kawaida. Ni jambo lisilo la kawaida sana, wakati anapotimiza Neno Lake kwa mwenendo wa kisasa wa siku hizi, maana mwelekeo wa kisasa wa siku hizi hauliamini. Wana njia yao wenyewe.

26 Sasa, tunaona, na hebu turudi kwenye Maandiko na kuchukua matukio mengine yasiyo ya kawaida, kwa dakika chache zaidi, wakati Mungu alipotimiza unabii Wake. Mungu anaposema jambo lo lote, Yeye atalifanya. Mbingu zote na nchi zitapita, bali Neno hilo haliwezi kupita kamwe. Kwa hiyo kwa kawaida husababisha tukio, tukio lisilo la kawaida.

Tazama namna Neno la Mungu lilivyo kama jambo la mzaha kwa wa—watu wanaotarajiwa kuliamini, walakini ni geni sana hata wanalia kwa sauti, "Vema, ni nini hii? Ulipata wapi upuuzi huo? Huyu ni nani? Ni kitu gani hiki?"

Wakati, walipaswa kupiga makelele, "Hosana kwa Mfalme ajaye katika Jina la Bwana!" Lakini kulikuwako na kundi dogo tu linalofanya jambo hilo, kundi dogo tu.

Kwa miaka elfu nne ya unabii, kwa ajili ya jambo kuu sana ambalo linaloweza kutokea kwa taifa, kwa kuwa tumaini lote la waliokufa lilitegemea Hiyo, wakati wao wote ujao ulitegemea Hilo; na wale watu wa dini, waliodai eti waliiamini, walikuwa wakipaza sauti, "Ni Nani? Na mvuto huu ni nini?" Kitu kisicho cha

kawaida! Vivyo hivyo, halibadiliki, sasa si la kawaida.

27 Hebu tuone baadhi ya mambo yasiyo ya kawaida, kama nilivyosema. Ni nini kilichovutia macho kabla tu ya hukumu kuupata ulimwengu na kuuangamiza kwa maji? Mzee mmoja, mwenye umri wa karibu miaka mia moja na ishirini, akijenga mashua wakati hakukuwa na maji ya kuelea ndani yake. Kule juu kwa miaka mingi, akisimama mlangoni, akijenga mle ndani, upande wa ndani, huku akiutia lami ndani na nje, na kusema, "Ulimwengu utamezwa na maji," katika wakati mkuu wa kisayansi.

"Je, ni nini kinachogongagonga kilimani kule juu?" "Mbona, ni mzee jina lake Nuhu, naye yuko huko juu, mzee mshupavu wa dini. Yule mzee alisimama juani kwa muda mrefu sana. Yeye amepatwa na jua. Amerukwa na akili. Naye anajenga kile anachoita 'safina,' na kusema maji yanatoka kule juu ambako hakuna maji, na yatawachukua watu wote humu,; na kila mtu asiyeusikia ujumbe wake, na kila mtu ambaye hataingia kwenye safina hiyo, atazamishwa maji. Uliwahi kusikia jambo kama hilo?" Ulikuwa ni mvuto usio wa kawaida!

28 Ninawazia wakati watu walipotaka kucheka vizuri, walipanda wakaenda na kusimama mbele ya mlango wa safina na kucheka. "Mbona, ulisema itanyesha miaka mia moja iliyopita! Babu aliniambia alikusikia hapa juu ukisema mvua itanyesha, nawe ungali unapigapiga juu ya kipande hiki cha mti hapa juu. Kwa nini usijitambua mwenyewe?"

Lakini ilikuwa ni Mungu akijitayarisha kuthibitisha ahadi na kutimiza unabii ambao nabii Wake alikuwa ametoa. Jambo lisilo la kawaida sana! Mungu akitimiza ahadi Yake kwa Nuhu, wakati wengine walikuwa wakicheka. Mungu pia alikuwa akijitayarisha kufanya historia kuwaonyesha wengine, hata siku hizi, ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake! Haidhuru linaonekana si la kweli iliyoje, na halina busara, Yeye angali hutimiza Neno Lake. Alikuwa akionyesha kwa mfano, kutokana na mzee huyo akiligongagonga sanduku hilo, kwa ajili ya watu hawa hapa Marekani usiku wa leo na kote ulimwenguni. Haidhuru sayansi inasema nini, wanasema nini, *hiki, kile*, ama *kinginecho*, Yeye angali hutimiza Neno Lake. Alikuwa akiandika historia.

29 Nini kilichokuwa kivutia siku moja; jambo lisilo la kawaida lilitukia huko nyuma nyikani, na lilikuwa ni kichaka kilichowaka moto. Na nabii mtoro alikuwa amesimama huko nyikani. Kamwe hakusikia sauti yoyote, kamwe hakusikia sauti yoyote, bali aliangalia na kuona jambo lisilo la kawaida juu ya mlima. Mungu alikuwa akijaribu kuvutia usikivu wake. Ndivyo ilivyo leo!

Mungu alikuwa akijitayarisha kulitimiza Neno Lake, kwa nabii Wake Ibrahimu, "Uzao wako utakuwa mgeni kwa muda wa miaka mia nne katika nchi ya kigeni. Nitawatoa kwa mkono wenye nguvu."

Naye alikuwa akimwandaa mtu kwa ajili ya kazi hiyo, kama alivyokuwa akiandaa safina kwa ajili ya mahali pa usalama kwa wote ambao wangeamini. Mungu alichoma kichaka hiki kwa moto, naye mchungaji huyu wa kondoo, Musa, akasema, "Nitageuka tu nione jambo hili la ajabu linamaanisha nini." Na alipomfanya Musa kukaribia kile kichaka,, alinena naye.

30 Mvuto ulikuwa nini baadaye katika ukumbi wa Pilato, wakati mchungaji huyu alipotupa fimbo chini na ikageuka kuwa nyoka? Mungu akitimiza ahadi Yake kwa Musa. Ni kitu gani kilichokuwa kivutio kwenye Bahari ya Chumvi, farasi wa Farao walipostangaa, walipoona upepo ukishuka kutoka mbinguni na kugawanya Bahari ya Shamu kutoka kulia hata kushoto; na maskini kundi la watumwa wakiwa wanaenda katika kazi ya Mungu wakavuka hiyo katika nchi kavu? Ilikuwa ni kitu gani? Mungu akitimiza Neno Lake. Mauti yaliondoka, watu walio hai wakavuka; na watu waliokufa kiroho walijaribu kuigiza, nao wakazama maji. Mungu akitimiza unabii na kuandika historia. Huo ulikuwa ndio mvuto kwenye Bahari ya Shamu.

31 Ni kitu gani kilichovutia siku ya pili baada ya hapo, kwenye Mlima Sinai, wakati watu wote walipoamriwa kutowafikia wake zao, wakati walipoambiwa wafue nguo zao na kujitakasa, na kukusanyika karibu na mlima ambapo mtu jina lake Musa alikuwa amesema alikutana na Mungu katika Nguzo ya Moto? Na Mungu alikuwa amemwambia Musa, "Nitashuka nije miongoni mwa watu. Nitahakikisha hayo niliyowaambia, na kwamba Mimi ni Nani. Nitawaonyesha ya kwamba Mimi ndiye Mungu yule." Huo ulikuwa ndio mvuto, Mungu akitimiza Neno Lake.

32 Nini kilichovutia siku moja katika historia, ambapo taifa fulani lilikuwa limemsahau Mungu, ambapo watu walikuwa wamekuwa baridi na wasiojali, ambapo makuhani wote walikuwa wameingilia mambo ya kisasa, manabii walitabiri kulingana na mapenzi ya makuhani? Na katika siku hiyo, kama kawaida, walikuwa na mtu mmoja ambaye walidhani alikuwa mshupavu wa dini. Alinena juu ya wanawake kupaka rangi, na kila kitu, naye alikuwa mtu wa kuchekesha. Na huyu mzee alikuwa ameshuka na kumwambia mfalme, "Hata umande hautaitwa…hautakuja hata nitakapouita."

33 Nasi tunatambua, basi, ya kwamba alikuwa amejificha na kukimbia, naye alikuwa amejificha jangwani mahali fulani. Watu walidhani ya kwamba labda alikuwa amekufa kwa njaa ama kuangamia; bali alikuwa amelishwa vizuri sana, na kumwagiliwa maji, pia. Na huyu hapa, akashuka na kusema, "Je! Mnaona ya kwamba nina BWANA ASEMA HIVI? Sasa, kama bado hujashawishika, hebu tupande juu ya kilele cha

mlima na kuthibitisha kwamba Mungu ni nani," kwa maana alikuwa na ono lingine kutoka kwa Bwana.

Akasema, "Jichagulieni madhahabu, mkaitayarishe, na—na mkachague ng'ombe dume mkawachinje. Nitafanya madhabahu ya Bwana, na pia nitaweka ng'ombe juu ya madhabau yangu. Sote tutatoa dhabihu, na kumruhusu Mungu aliye Mungu ajibu." Yeye hangefanya jambo hilo kamwe kama Bwana asingemwambia; alisema hivyo baadaye, "Nimefanya hili katika … haya yote, kwa amri Yako, Bwana."

34 Lakini ni nini kilichovutia? Mna makuhani mia nne waliosimama mlimani, naye mfalme yumo mle juu katika gari lake, pamoja na askari wake wote na walinzi waliomzunguka. Naye huyu mzee, mwenye nywele kama sufu, za kimbimbi, mwenye upara, na nywele zilizoning'inia usoni, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, nywele zimemjaa mwilini, huku amesimama na fimbo mkononi na chupa ya mafuta kwenye mkono mwingine, alikuwa amesema tu miaka mitatu na nusu hapo mbeleni, "Hata umande hautaanguka hata nitakapo…nitakapouagiza" akichukua mahali pa Mungu, pamoja na vitu kama duara ya mwanga na vivuli na yote wanayonena habari zake. "Na hapa yule mzee mshupavu wa dini amesimama pale juu ya kilima, akiwaleta watu hawa wote kule juu." Ni nini kilichovutia? Ilikuwa ni Mungu akijiandaa kumthibitisha nabii Wake kuwa sahihi. Ilikuwa ni Mungu akitimiza unabii. Mungu pia akiandika historia, akitimiza Neno.

35 Miaka mia chache baada ya hapo, kulikuwako na mtu aliyetiwa mafuta na Roho yeye yule, naye alitoka nyikani, hajaungana na madhehebu yo yote; ingawa baba yake alikuwa mtu wa madhehebu, kuhani wa utaratibu fulani. Bali alitoka nyikani, amevaa ngozi ya kondoo, amevaa nywele usoni mwake. Badala ya kuwa zenye mvi, zilikuwa nyeusi. Ni kitu gani kilichomvutia mtu huyu kilichovutia Yerusalemu yote na Uyahudi? Baadhi yao wakitoka na kusema, "Kuna mtu wa nyikani kule chini. Yeye anajaribu kuwazamisha watu majini. Ni nani aliyepata kusikia jambo kama hilo?"

36 Wengine walikuwa wadadisi, na kusema, "Huyu lazima ndiye Masihi." Mmoja wao alisema, "Huenda ikawa ni mmoja wa manabii." Hawakujua la kuwazia. Lakini ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni Mungu akitimiza Isaya 40, ambapo Yeye alisema, "Tazama …" yale angefanya katika siku za mwisho, namna angemtuma mtumishi Wake na yale angefanya.

Ndipo tunaona, majuma machache baada ya hayo, mtu huyo akiwa na hakika sana na ujumbe wake, hata akasema, "Kuna Mtu anayesimama katikati yenu, ambaye sistahili kuvichukua viatu vyake. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto, kama vile nilivyobatiza kwa maji."

37 Siku moja Kijana wa kawaida, mwenye umri wa kama miaka thelathini, alishuka akaenda kubatizwa. Na wakati Mtu huyu alipokuja, kulikuwako na mvuto mkubwa sana kwa nabii, nabii alitenda mambo ya ajabu siku hiyo. Kusanyiko lisingeweza kujizuia kuangalia matendo ya nabii huyo.

Wakati alipokuwa akijadiliana na makuhani ng'ambo ya mto, walisema, "Mungu alijenga madhabahu hii. Mungu alitwambia tufanye hivi. Musa ni nabii. Tunamwamini Musa. Sadaka ya kuteketezwa hiyo haitaondolewa kamwe."

Ninaweza kumsikia Yohana akijibu, kasema, "Hivi hamjasoma katika Maandiko yale nabii Danieli aliyosema, 'Sadaka ya kuteketezwa ya kila siku itaondolewa'? Na wakati huo umewadia! Hivi hamjasoma yale Isaya aliyosema katika mlango wa 40, 'Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana'? Hao ni manabii mawili kwangu. Na jambo lingine, hivi hamkumtambua nabii wetu miaka mia nne iliyopita, Malaki, wakati aliponena katika mlango wa 3 na kusema, 'Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia'? Hivi hamjui jambo hili linatimiza unabii?" Unabii ulikuwa ukitimizwa!

38 Na yapata wakati huo nabii aligeuka na kusema, "Tazama, yuaja Mwana -Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" Sasa mvuto ni nini? Imebadilishwa kutoka kwa nabii ikawa unabii wake.

Sasa angalia kinachotukia. Huyu hapa anakuja Mtu wa kawaida, asiyejulikana na mtu yeyote, mwana wa seremala, akija akitembea majini. Wakati Yohana, yule nabii mkuu, aliposema, "Ninahitaji kubatizwa na Wewe. Mbona unakuja kwangu?"

Yeye alisema, "Kubali iwe hivyo. Lakini, kama nabii na Neno, inatupasa kutimiza haki yote."

Kwa hiyo akaelewa Dhabihu ilibidi ioshwe kabla haijatolewa, naye akambatiza.

39 Sasa kuna mvuto mwingine unaotendeka wakati alipotoka majini. Nabii huyu ambaye alikuwa mwaminifu sana kutangaza wakati wake na wakati, aliangalia juu na kuona mbingu zimefunguka. Alimwona Roho wa Mungu, kama hua, akishuka juu Yake, na Sauti ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu ninayependezwa Naye." Mungu alikuwa akithibitisha ujumbe wa nabii, kile kilichokuwa kinavutia usikivu huko Yordani.

40 Ndugu aliimba muda mfupi uliopita, ama alipaswa kuimba, "Kilimani mbali sana mlisimama Msalaba wa kale unaoparuza." Kuna mvuto gani juu ya Mlima Kalvari? Tunapoona ulimwengu wa kidini ulikuwa

umemhukumu, na serikali ya Kirumi ilikuwa imemhukumu kifo. Na hapa Yeye alikuwa akining'inia kati ya wahalifu wawili, akifa kwa kiu, Damu ikitiririka mwilini Mwake. Huyo hapo ananing'inia, akilia, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Nao watu wa kidini waliosimama pale, wakiuangalia, hawakujua ya kwamba unabii wa Agano la Kale ulikuwa ukitimizwa pale pale Kalvari wakati huo.

Daudi mwenyewe aliandika, akatenda…akaingia katika Roho kama manabii wote, akatenda kama kwamba ilikuwa yeye. Daudi alilia, katika Zaburi ya 22, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Mifupa Yangu yote wananiangalia. Waliichoma mikono Yangu na miguu Yangu." Daudi, akinena kana kwamba ni yeye. Na haikuwa Daudi, ilikuwa ni Kristo katika Daudi.

Na hapa unabii wenyewe uliotoka, wa manabii mbalimbali, ulikuwa ukitimizwa juu ya Mlima Kalvari. Kuna mvuto gani juu ya Mlima Kalvari? Mungu akitimiza Neno Lake.

41 Kivutio kingine kilikuwa juu ya mlima, ilikuwa ni kwenye Siku ya Pentekoste, wakati hao wote walikuwa huko juu kwenye karamu ya kidini, walidhani walikuwa wamewaondoa washupavu wote wa dini. Hawakuwa wamesikia kutoka kwao kwa siku kumi. Kwa ghafula, kama mzinga wa nyuki, wakatokea juu ya jengo, wakaingia mitaani, wakipiga mayowe na kupiga makelele.

"Ni kitu gani hiki? Nini maana ya jambo hili? Je! Watu hawa wote wamelewa?"

Angalia! Ndipo nabii akasimama miongoni mwao, jinsi taratibu za nabii zinapaswa kuwa, na akasema, "Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi mkaao Yerusalemu na Judea, lijueni jambo hili, mkasikize maneno yangu. Watu hawa hawakulewa kama mnavyodhani wamelewa. Lakini jambo hili ni lile lililonenwa na Bwana kwa Yoeli, nabii, 'Itakuwa siku za mwisho, nitamwagia watu wote Roho Yangu." Huo ulikuwa ndio mvuto.

42 Watu wa dini, baada ya kumsulubisha Mfalme wa Uzima, na kila kitu, bado hawakuona ahadi ya kuja kwa Roho Mtakatifu. Mvuto huo, "Ni nani huyu? Hii ina maana gani? Watu hao wana shida gani?"

Loo, jamani! Ni vivyo hivyo leo. Tutavuka mambo mengi ya hili kusudi tukailete kwa saa hii. Ni jambo lile lile ni leo. Jambo lile lile linatukia. Swali lile lile linaulizwa. "Shida hizo zote ni nini?" Tazama huku na huko barabarani, magari kutoka Michigan hadi Florida, kutoka Maine hadi California. Asubuhi ya leo nilipokuwa nikiondoka, ama alasiri tulipokuwa tukitelemka barabarani, mimi na mke wangu tulikuwa tukichunguza leseni za motokaa. Hapo ndipo nilipolifikiria somo hili.

"Hii ina maana gani?"

Kama tu vile ilivyosema, "Palipo na Mzoga, ndipo tai watakusanyika."

43 Nikamwambia mke wangu, "Mpenzi, unakumbuka usiku uliopita wakati ilinilazimu kuagana na kila kitu nilichokipenda duniani, na kuenda kule nje kuanzisha kitu ambacho Mungu alisema nifanye? Uliimba ule wimbo."

Loo, watatoka Mashariki na Magharibi,
Walitoka nchi za mbali,
Kula pamoja na Mfalme wetu, kula kama mgeni Wake;
Jinsi wasafiri hawa walivyobarikiwa!
Kuangalia uso Wake mtakatifu
Inawaka kwa upendo wa Kiungu;
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Kama vile vito katika taji Yake vitakavyoangaza.

44 Hivyo ndivyo mvuto ulivyo. Uzao wa Mungu uliochaguliwa tangu asili ambao hauwezi kufanya jambo lingine ila kulifuata, unamaanisha zaidi ya uhai kwetu. Twaa maisha yetu, bali usichukue Huo. Mvuto ni nini? Mungu, kama kawaida, akitimiza Neno Lake. Yeye anatimiza Neno la Zekaria tena, la nabii Zekaria.

Ambapo nilisoma kifungu cha 9 muda mfupi uliopita, wakati Yesu alipoingia hekaluni Mwake, akipanda … ama aliingia Yerusalemu, amepanda punda mdogo, mweupe, unabii ulitimia ambao Zekaria alisema. Hili hapa, "Furahini sana, enyi binti za Sayuni. Pigeni kelele, enyi binti za Yerusalemu. Tazama, Mfalme wako anakuja kwako; Yeye ni mwenye haki, na ana wokovu; mnyenyekevu, amepanda punda, na mwana punda mwana wa punda." Hivyo ndivyo mvuto ulivyokuwa huko Yerusalemu, kwenye makao makuu ya kidini.

45 Sasa tunaona tukio la siku za mwisho likitukia! Hebu na tufungue kurasa chache tu, katika Zekaria, na tuone kile alichosema juu yake. Hebu na tulifungue basi kwa ajili ya siku za mwisho. Huo ulikuwa wakati wa katikati; hebu tugeukie sasa siku za mwisho. Na tufungue Zekaria, mlango wa 14, na kuanzia kifungu cha 4. Na sikilizeni! Nasi tutasoma sehemu ya Maandiko, kama aya tisa, kutoka 4 hadi 9. Sikilizeni kwa makini. Na ni kutabiri juu ya Kuja Kwake, siku za mwisho. Sikilizeni kwa makini sasa. Hii ni BWANA ASEMA HIVI. Ni Maandiko, Zekaria 14. Kumbuka Zekaria 9, kile ilichosema? Nao hawakulitambua. Sasa ni kitu gani leo? Zekaria 14, akinena juu ya Kuja Kwake.

*Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki, nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake, upande wa mashariki na upande wa magharibi; litakuwako huko bonde kubwa sana; ... na nusu ya mlima ule utaondoka kwenda upande wa kaskazini, na nusu yake ... itaondoka kwenda upande wa kusini.*

*Nanyi mtakimbia kwa njia ya bonde la milima yangu; kwa maana bonde lile la milima litaenea hata Aseli; naam, mtakimbia, kama vile mlivyokimbia mbele ya tetemeko la nchi, siku za Uzia, mfalme wa Yuda; ...*

46 Tetemeko lingine la ardhi likiipasua dunia! Kama unataka kufuata Andiko hapa, angalia katika kifungu hiki cha 5, inahusu kwamba kutengana kwa Mlima wa Mizeituni kunatokana na tetemeko la nchi, na hili linathibitishwa na Isaya 29:6 na Ufunuo 16:9. Kweli kabisa! Ni kitu gani? Nabii yule yule alisema juu ya kuja Kwake mara ya kwanza, aliona Kuja Kwake mara ya pili. Angalia, "Kama katika siku za tetemeko la nchi." Mnaona yale matetemeko ya nchi yanavyofanya? Unaona utabiri wao?

*... NA BWANA, Mungu wangu, atakuja, na watakatifu wote pamoja naye.*

*Na itakuwa katika siku hiyo, (haleluya) katika siku hiyo, ya kwamba nuru haitawaka, wala giza;*

*Lakini itakuwa siku moja, ... iliyojulikana na Bwana; si mchana, wala si usiku; lakini itakuwa, ya kwamba wakati wa jioni kutakuwako nuru.* (Ee Mungu!)

47 "Itakuwa Nuru wakati wa jioni," nabii yule yule. Nao watu ni vipofu! Ni kivutio gani? Hebu tusome vifungu kadhaa zaidi.

*Tena itakuwa siku hiyo, ya kwamba maji yaliyo hai yatatoka katika Yerusalemu; nusu yake itakwenda upande wa bahari ya mashariki, na nusu yake ... upande wa bahari ya magharibi; wakati wa hari na ... wakati wa baridi itakuwa hivi. (Injili ikihubiriwa; Wayahudi na Mataifa pia.)*

*Naye Bwana atakuwa Mfalme juu ya nchi yote; siku hiyo BWANA atakuwa mmoja, na jina lake moja.*

Itakuwa Nuru wakati wa jioni, (kulia)
Njia ya Utukufuni hakika mtaipata;
Katika njia ya maji kuna Nuru leo,
Kuzikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia;
Nuru ya jioni imekuja,
Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.

Mnaona mahali tulipo?

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo manabii wetu walitabiri; (lile tetemeko la nchi kwa Mataifa hata siku ya mwisho)
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;
Rudini, enyi mliotawanyika, nyumbani kwenu.

Ninyi mliofukuzwa, na visanduku hivi vilivyobebwa katika magari mapya, tokeni huko kabla mauti hayajawapata. Mungu amelithibitisha. Itakuwa hivyo.

48 Hebu na tufungue kwenye Andiko lingine katika Agano la Kale, Malaki sura ya 4, na tusome hiyo sura ndogo ya 4.

*... angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, ... wote watendao uovu, watakuwa makapi; ...*

Sasa, hii si … Hiyo ni Malaki 3, ilikuwa ni kuja kwa kwanza, sasa huku kuna kuja kwingine. Hata Daktari Scofield hapa, hakika sikubaliani naye katika maelezo yake, bali ameziandika hapa vizuri. "Agizo la Yohana," kwa Malaki 3; na, "Kuja kwa pili kwa Kristo," na Eliya kabla. Vema.

*... wote wenye kiburi, itawateketeza, asema BWANA wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi.* (Iko wapi kuzimu ya "Milele"?)

*Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; ... nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini.*

*Nanyi mtawakanyaga waovu; ... maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu;*

*katika siku ile niifanyayo, asema Bwana wa majeshi.*

*Ikumbukeni ... torati ya Musa, mtumishi wangu, niliyomwamuru ... huko Horebu kwa ajili ya Israeli wote, ... naam, amri na hukumu.*

49 Hapa kuna kuja kule kwa Eliya.

*Tazama, nitawapelekea Eliya nabii …*

Andiko la mwisho la kumalizia Agano la Kale!

*... Nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya.*

Sasa, huyo asingeweza kuwa ni Yohana. La. Mnaona, ulimwengu haukuchomwa moto na watakatifu kuwakanyaga waovu. Mnaona? La, la.

*… Kabla ya siku ile ya BWANA, iliyo kuu na ya kuogofya;*

*Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, nisije nikaipiga nchi kwa laana.*

Tazama usahihi wa Roho Mtakatifu, ya kwamba haingeweza kutatanisha kule kuja kuwili kwa Eliya. Malaki 3, ilisema, "Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu." Yesu aliulizwa habari za Yohana, Akasema, "Ikiwa tunataka kukubali, huyu ndiye manabii waliyesema, 'Nitamtuma mjumbe Wangu mbele Yangu.' Huyu ndiye Eliya atakayekuja." Malaki 3.

50 Angalia Maandiko yanatoa jambo hilo kwa usahihi sana. Tazama vile hili…kuonyesha yale…wale wanaotaka kuamini, wale wanaotaka kuona. Kumbukeni, Yesu akikoma katikati ya Maandiko, maana sehemu yake ilitimizwa wakati huo, hayo mengine kwa ajili ya Kuja Kwake mara ya pili? "Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa, kuwaganga waliovunjika moyo", kisha akakoma; si "kuleta hukumu juu ya Mataifa" hata Kuja Kwake mara ya Pili.

51 Angalia Andiko hili hapa linalingana na hilo. *"Naye, Eliya, ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao."* (Sasa, tukinena kuhusu Malaki 4, usiichanganye, ama Malaki 3.) Yohana, Eliya, aliyekuja katika zile siku kabla kule kuja kwa Kristo mara ya Kwanza, aligeuza mioyo ya wale wazee wetu wa kale kuelekea ujumbe wa watoto wao, ujumbe mpya.

Sasa angalia. "Na mioyo ya watoto kwa baba zao." Katika kuja kwake mara ya pili, katika siku za mwisho, anarudi kwenye Imani ya kimitume tena. Mnaona jinsi Maandiko yanavyopatana kikamilifu?

Huo ulikuwa ndio mwisho wa Agano la Kale, Agano la Kale. Sasa tunaona kuna Nuru wakati wa jioni. Ni kitu gani? Ni kilele, Mlima wa Kilele.

52 Kama nilivyosema asubuhi ya leo, tumekuja kupitia madhehebu, kupitia (si mchungwa) kama nilivyonena asubuhi hii, bali tumekuwa na balungi, ndimu, namna ya vitu vingine vyote ambavyo havikuwa hivyo kamwe tangu mwanzo. Lakini baada ya … Usilikose. Hili hapa laja. Baada ya madhehebu yote kumalizika, hawakuwa na Nuru yo yote tangu mwanzo, kutakuwako na siku ambayo haiwezi kuitwa mchana wala usiku.

Wanafanya nini? Wanafanya nini? Ninii—limao hufanya nini kwenye mti wa chungwa? Inahitaji uhai asili wa chungwa linalokua na kuupotosha kuwa limao. Hivyo ndivyo madhehebu yamefanya kwa Neno la Mungu, kulitangua Neno la Mungu kwa mapokeo yao. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Wamezaa malimao, mabalungi, si machungwa.

53 Lakini nabii alisema nini? Yule yule aliyesema katika somo letu usiku wa leo, "Furahi, Ee binti Yerusalemu, shangilia kwa sauti kuu, binti Sayuni, kwa maana Mfalme wako anakuja kwako, mpole na mnyenyekevu, amepanda mwana-punda, mtoto wa punda," tazama ya kwamba nabii yule yule alisema, "Kutakuja wakati wa kuivisha." Jua linatumwa juu ya nchi kuivisha tunda. Kwa nini haikuweza kuiva? Hakuna tunda pale la kuiva. Lakini ule Uzima ungali unaendelea.

54 Ulipanda kupitia balungi, liwe chungwa, tukapata kwamba ilifanyika dhehebu; ilikuwa ni balungi. Ulienda tena, ukatokea wakati huo ukiwa limao. Ukaendelea tena, ukawa kitu kingine. Na mwishowe, juu ya mti ikageuka kuwa tunda la tangelo, ambalo ni nusu chungwa na nusu limao; uzao uliochanganyikana; kitu kilichopotoshwa, ikafikia upotovu, likiishi kwa mti ule ule; kapi, "nusura iwapotezea walio Wateule." Inaonekana kama chungwa, bali sivyo.

"Bali kutakuweko Nuru," linapositawi kushinda madhehebu. Linapopita madhehebu na kusitawi tena, litazaa machungwa kama lilivyokuwa lilipoingia ardhini.

Nini hiki kinachovutia, ni nini kinachotendeka? Kutimiza Neno la Mungu. Kuna mashahidi wawili wa Agano la Kale, kwamba hili lingetukia.

55 Hebu na tuchukue Yohana 14:12, ya Agano Jipya, Yesu alisema.

> *… Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya; …*

Pia, katika Luka 17:22 hadi 30, Yeye alisema.

> Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, kabla ya Sodoma, kuteketezwa, ndivyo itakavyokuwa wakati wa kurudi kwa Mwana wa Adamu, *siku ile atakapofunuliwa Mwana wa Adamu.*

Loo, angalieni tu Maandiko! "Mwana wa Adamu," Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, alikua akiyapita madhehebu, akakulia juu ya ule Mti. Yeye alisema nini katika Yohana 14, au 15? "Kila tawi ndani yangu lisilozaa tunda, litakatiliwa mbali na kukatwa, likatupwa motoni na kuchomwa. Lakini kila tawi litakalozaa matunda, litatakaswa."

56 Naam, kutakuweko mvua ya kweli ya masika na ya vuli katika siku za mwisho juu ya hilo kundi dogo lililoambatana Naye alipopanda maskini punda yule, nyenyekevu na pole, lisilo na nini ... wala dhehebu, likilia, "Hosana, Mfalame ajaye katika Jina la Bwana!" Kuna nini leo? Kuna mvuto gani mlimani?

57 Si muda mrefu uliopita, nikiwa nimesimama kwenye mimbara hii, ilisemwa na Roho Mtakatifu, "Siku itakuja ambapo watapiga kigingi mbele ya nyumba yako; watasogeza lango lako. Kwa hivyo, hayo, hutayajali na usikasirike." Niliona lango langu limevujiliwa mbali na kutupiliwa kilimani. Niliona kile kilima mbele zangu kimelimwa chote, mbao na vinginevyo vilikuwa kule ambako kitu fulani kilivivunjilia mbali. Yeye alisema …

Nikaangalia, na kulikuwako na Ricky mdogo aliyeenda kule na kuvunja-vunja lile lango, akafanya hili. Nikasema, "Kwa nini hukuniambia?" Alikuwa mwerevu kwangu, nami ilinibidi kumpiga. Na nilipofanya hivyo, nikasema, "Sijafanya hivi tangu nilipokuwa mwanandondi, bali nataka tu kujua," nami nikampiga konde moja. Na wakati nilipomwangusha chini, nikamchukua tena na kumwangusha chini tena. Nami nikamwinua mara tatu nne, na ndipo nikampiga na kumtupa upande mwingine wa kilima kile. Kwa hiyo basi nikaenda kule, na kusema, "Hiyo si sahihi." Nami nikamchukua na kumpa mikono, nikasema, "Sina hasira nawe, bali nataka tu ujue huwezi kuzungumza nami namna hiyo."

Halafu basi nilipogeuka na kurudi, Roho Mtakatifu alikuwa amesimama pale langoni, akasema, "Sasa kwepa hili. Wakati kile kigingi kinapopigiliwa chini, geukia upande wa magharibi."

> Kitabu hiki, ndicho kila kitu ninachohitaji,
> Kitabu hiki ni Maelezo mazuri,
> Kwa namna ambavyo kinaonyesha jinsi ninavyoweza kuepuka shida yangu.
> Amina!

Na hicho Kitabu ni Neno, na Neno hilo ni Mungu. Usijali shida zako, kitakwambia utakayofanya.

58 Miaka mitatu iliyopita nilimsikia rafiki yangu, mpimaji wa jiji, anaishi kwenye upande mwingine wa barabara kutoka kwangu, akipigilia kigingi chini. Nilitoka nikaenda kule na kusema, "Kuna nini, Tope?" Mwana wa Bw. King, rafiki msiri wangu.

Kasema, "Billy, wataipanua barabara hii."

Nyote mnakumbuka. Nikasema, "Huenda ikawa ndiyo lile daraja." Nilimwambia Ndugu Woods, nikasema, "Shikilia mali yako. Labda daraja hilo litapitia hapa juu, kitu fulani." Njia hiyo ilikuwa imeraruliwa; matofali, miamba, ilitupwa juu ya kila kitu. Kwa hiyo akasema … Nikasema, "Shikilia mali yako." Ndipo wakati mimi …

Bw. King aliniambia hilo lingetukia.

Nikaingia, nikamwambia mke wangu anayeketi pale, "Mpenzi, kuna kitu kilichoandikwa kuhusu jambo hilo. Ni BWANA ASEMA HIVI, mahali fulani."

59 Niliingia na kuchukua kitabu changu, nikakichunguza, na kasema, "Itakuwa …" Miaka minane baadaye!

Ndipo nilipoliangalia, nikasema, "Wakati umewadia sasa, mpenzi, hatuna budi kuelekea magharibi."

Siku mbili baada ya hapo, nikiwa nimesimama chumbani yapata saa nne asubuhi moja, niliingia katika Roho wa Mungu. Niliona lile kundi la hua likiruka, nikawaangalia hao ndege wadogo. Mnakumbuka jambo hilo. Niliwaona Malaika saba katika umbo la piramidi, wakija kwa haraka wakinijia. Kasema, "Geukeni magharibi, mwende Tucson, mwe maili arobaini kaskazini mashariki. Nawe utakuwa ukijitoa gugu fulani" ama, huitwa kichwa cha fahari "kutoka nguoni mwako."

60 Ndugu Fred Sothmann, anayeketi pale akiniangalia sasa hivi, alikuwa pale asubuhi hiyo. Nilikuwa nimesahau jambo hilo.

Nikasema, "Mlipuko ulitokea kama tetemeko la ardhi, ambalo lilitikisa karibu kila kitu kilichokuwako nchini. Sioni namna mtu angaliweza kuishi." Niliogopa. Nilisimama huko Phoenix, ninyi nyote mnaosikiliza usiku wa leo nishuhudieni. Nilihubiri mahubiri, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* "Tuko wapi?" Nilienda Magharibi. Wengi wenu hapa mlipata kanda hiyo, wengi wenu hapa mlisikia ikisemwa, mwaka mmoja au zaidi kabla haijatukia.

61 Nikaenda Magharibi, nikishangaa kile kitakachotukia. Siku moja nilipata mwito kutoka kwa Bwana. Nilimwambia mke wangu, nikasema, "Mpenzi, mimi … labda kazi yangu imekwisha." Sikujua. Nikasema, "Mimi … Mungu, labda Mungu amemaliza na mimi sasa nami nitaenda nyumbani. Nenda zako pammoja na Billy, uwachukue watoto. Mungu atakufanyia njia, kwa namna fulani. Nenda zako ukaishi mwaminifu kwa Mungu. Angalieni kwamba watoto wanamaliza shule, ukawalee katika maonyo ya Mungu."

Yeye akasema, "Bill, hujui—hujui kama hiyo ni kweli."

Nikasema, "La. Lakini mtu asingeweza kustahimili jambo hilo."

Na asubuhi moja Bwana aliniamsha, kasema, "Nenda kule juu kwenye Magenge Marefu ya Sabino." Nilichukua kipande cha karatasi na Biblia yangu.

Mke akasema, "Unaenda wapi?"

Nikasema, "Sijui. Nitakwambia nitakaporudi."

62 Nikapanda juu kwenye magenge, nikapanda moja kwa moja ambako tai walikuwa wakiruka huku na huko. Nilikuwa nikimwangalia kulungu fulani amesimama pale. Nikapiga magoti kuomba, nikainua mikono yangu, na Upanga ukauangukia mkono wangu. Nikaangalia kila mahali. Nikawaza, "Ni kitu gani hicho? Sijapatwa na kichaa. Hapa mna ule Upanga mkononi mwangu, mwangavu, unaong'aa, unametameta juani." Nikasema, "Sasa, hamna watu kwa maili nyingi kutoka hapa nilipo kwenye magenge haya. Huo ungeweza kutoka wapi?"

Nikasikia Sauti, ikasema, "Huo ni ule Upanga wa Mfalme."

Nikasema, "Mfalme ye yote humpandisha mtu cheo kwa upanga."

Yeye yule Sauti akarudi, kasema, "Si upanga wa mfalme," bali 'Ule Upanga wa Mfalme,' Neno la Bwana." Kasema, "Usiogope. Ni ule Mvuto wa Tatu tu. Ni thibitisho la huduma yako."

63 Nilikuwa nikienda kuwinda pamoja na rafiki yangu, bila kujua kitakachotukia.

Na mtu fulani akanipigia simu, ambaye alinilaumu kwa ajili ya ile picha ya Malaika wa Bwana, ambayo aliipiga. Ilinilazimu kwenda Houston kwa ajili ya mwanawe, kwa maana alikuwa akielekea kwenye maangamizi naye angekufa katika muda wa siku chache. Naye akakutana nami mle ndani na kunikumbatia, akasema, "Wazia, mtu yule yule niliyemkosoa anakuja kumwokoa mwanangu wa pekee!" Chama cha masilahi ya binadamu kikanitunza nishani inayoitwa Oscar, ama cho chote unachotaka kuiita, kwa ajili ya kuokoa maisha.

64 Ndipo tukarudi, nikaenda mlimani kuwinda. Na hapo Ndugu Fred na mimi, asubuhi moja nilipoondoka, tayari nilikuwa nimempata javelina wangu, na nikatazama na kuona mahali alipokwenda. Nikasema, "Ndugu Fred, nenda kwenye mlima huo asubuhi na mapema sasa, karibu na mapambazuko, nami nitapanda ule mwingine. Sitampiga risasi yule nguruwe mwitu, sitamuua. Lakini kama wakianza upande huu, kundi hilo, nitawapiga risasi mbele yao na kuwarudisha nyuma."

65 Ndugu Fred alitoka akaenda kule wala hakukuwa na nguruwe mwitu. Alinipungia mkono nikaona. Nikatelemka katika yale magenge, mashimo makubwa sana, jua lilikuwa likichomoza. Nikazunguka upande mwingine wa kile kilima, bila kufikiria cho chote juu ya ule unabii. Nikaketi chini, nikingoja, nikipumzika, nikawazia, "Imekuwaje kwa wale nguruwe mwitu?"

Nikachukua … Nikaketi jinsi Wahindi huketi, mwajua, kupitanisha miguu, nami nikaangalia mguu wa ovaroli yangu na ilikuwa na mbegu ya kwekwe. Nikaichukua. Nami nikasema, "Hilo ni jambo la ajabu! Niko hapa, yapata maili arobaini kaskazini mashariki mwa Tucson. Yule mtoto wangu mdogo Joseph ameketi pale akiningojea." Na mara nilipoanza kutazama, nikaona kundi la nguruwe mwitu yapata yadi elfu moja kutoka kwangu, juu mlimani, nami nikatupa ile mbegu ya kwekwe chini. Nikasema, "Nitawapata. Nitaenda nimwite Ndugu Fred, nami nitatundika kipande cha karatasi kutujulisha tupitie wapi, kwenye mzingile mwambije huu hapa, nasi tutampata Ndugu Fred."

Nami nikaanza kupanda mlima, nikikimbia sana niwezavyo upande ule mwingine. Kwa ghafla, nilifikiri mtu fulani alinipiga risasi. Sikuwahi kusikia mlipuko kama huo; ulitikisa nchi nzima. Na, ilipotendeka, mbele yangu kulikuwa na Malaika saba katika kundi.

66 Nilikutana na Ndugu Fred na hao wengine, baadaye kidogo. Kasema, "Ilikuwa ni nini?"

Nikasema, "Hiyo ilikuwa ndiyo."

"Utafanya nini?

"Rudi nyumbani. Kwa kuwa, BWANA ASEMA HIVI, zile siri saba ambazo zimefichwa katika Biblia miaka hii yote, madhehebu haya na kila kitu, Mungu atatufungulia hizo siri saba katika zile Muhuri Saba."

Kulikuwako na duara hiyo ikipanda juu kutoka ardhini, kama ukungu unaofanyika. Ulipofanya hivyo, ukapanda moja kwa moja juu ya mlima kabisa, ukaanza kuzungukazunguka pande za magharibi jinsi ulivyokuja. Sayansi iliupata baada ya kitambo kidogo, maili thelathini kwenda juu na maili ishirini na tano kwa upana, katika mzunguko wa piramidi kabisa.

67 Na hivi majuzi, nilipokuwa nimesimama pale, nikaigeuza ile picha upande wa kulia, Yesu akaonekana mle jinsi alivyokuwa katika zile Nyakati Saba za Kanisa, mwenye kufunikwa nywele nyeupe, ikionyesha Uungu Mkuu. Yeye ni Alfa na Omega; Yeye ni wa Kwanza na wa Mwisho; Yeye ndiye Hakimu Mkuu wa Umilele wote, akisimama pale kuthibitisha Ujumbe wa wakati huu. Na kutakuwako Nuru wakati wa jioni! Je, maana yake yote ni nini? Ilikuwa ni kitu gani?

68 Nikaenda upande wa magharibi. Juu ya mlima ule ule, nikipita pale pamoja na Banks Wood pale, kasema, "Tupa jiwe hewani. Mwambie Bw.Woods, 'BWANA ASEMA HIVI, utauona Utukufu wa Mungu.'"

Kesho yake, tukisimama pale, upepo wa kisulisuli ulishuka na kulipua milima. Majabali yalikatilia mbali vilele vya miti, yapata futi tatu nne juu ya kichwa changu. Ukasababisha milipuko mitatu mikubwa, na ndugu wakanikimbilia. Kulikuwa na watu kama kumi na watano waliosimama pale, wahubiri na kila kitu kingine. "Ilikuwa ni nini?" Akasema, "Ilikuwa ni nini?"

Nikasema, "Hukumu inaipiga Pwani ya Magharibi."

69 Yapata siku mbili baadaye, tetemeko la nchi nusura lizamishe Alaska. Je, hii Nuru juu ya Mlima Sunset katika Msitu wa Coronado wa Arizona ni nini? Je, kitu hiki cha ajabu kilichotokea kule juu, ambacho watu wamekuwa wakisafiriri kuelekea mashariki kutokea magharibi, wakiokota miawe yaliyotawanyika pale Hiyo ilikopiga? Na kila moja yao, kila moja ya majabali hayo, lina ncha tatu, lilizopasua. (Hao watatu ni Mmoja.) Yamewekwa kwenye madawati, yanawekwa juu ya karatasi, kote nchini. Je, ni jambo gani hili la ajabu juu ya Mlima Sunset katika Msitu wa Coronado?

70 Junior Jackson unasikiza, unakumbuka ile ndoto aliyokuwa nayo ambayo niliifasiri, "kuelekea kwenye machweo ya jua"? Na hili lilitukia kwenye Mlima wa "Sunset". Ni wakati wa jioni, wakati wa machweo. Ujumbe wa machweo kwa machweo ya historia, machweo ya unabii, hasa, ukitimizwa. Na itakuwa Nuru wakati wa jioni, juu ya Mlima Sunset katika Msitu wa Coronado, maili arobaini kaskazini mwa Tucson. Ingia kwenye ramani uone kama kilele cha Sunset pale. Hapo ndipo hasa ilipotukia. Kamwe sijui jambo hilo mpaka hivi majuzi.

71 Kila kitu ambacho … Hilo halitakufa kamwe. Inaendelea kujifungua kila wakati. Kutoka kwenye jambo lile lile linalotukia, hadi kwenye picha akiwa Yesu amesimama akituangalia; na sasa hasa kwenye Mlima wa Sunset, na Nuru ya machweo ya jua. Nuru ya jioni imekuja, Mungu akijithibitisha Mwenyewe. Ni kitu gani? Ni ukweli kwamba Mungu na Kristo ni mmoja. Kile "cheupe." Wangapi wamepata kukiona, zile nywele nyeupe juu Yake, kama tulivyonena katika Ufunuo 1? Mnaona, Uungu Mkuu, Mamlaka Kuu; hakuna sauti nyingine, hakuna mungu mwingine, hakuna kitu kingine! "Katika Yeye unakaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili." Malaika Wenyewe walikuwa ni wigi Yake. Amina.

72 Nini kimetukia juu ya Mlima Sunset? Mungu akithibitisha Neno Lake. Hiyo ndiyo sababu ya kelele hizi zote. Tazama, ni Mungu akitimiza Neno Lake lililoahidiwa tena, la Ufunuo 10:1 hata 7, "Na katika siku za kupigwa baragumu ya Ujumbe wa malaika wa saba, hapo ndipo siri ya Mungu inapaswa kutimizwa." Siri iliyofichwa ya Ufunuo 10:1 hadi 7, Ujumbe wa mwisho kwa wakati wa mwisho wa kanisa. Inatimiza kabisa, katika wakati huu, Luka Mtakatifu 17:30, "Siku atakapofunuliwa Mwana wa Adamu."

"Na watatokea manabii wa uongo na Makristo wa uongo, wataonyesha ishara kuu na maajabu, hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Watu wangali wana mashaka. Na, kama kawaida, kanisa linashangaa vile vile.

73 Na sayansi kote katika Tucson, wangali wanaandika makala madogo madogo na kuyaweka magazetini. Kule nyuma mbali sana juu ya Mlima Lemmon, zile kamera kubwa hazikuiona ikiinuka kutoka mahali tulipokuwa tumesimama; ikipeperukia upande wa magharibi, ikionyesha ya kwamba wakati umekwisha. Haiwezi kusonga tena isipokuwa mahali padogo sana, iko kwenye Pwani ya Magharibi. Hukumu ilitokea tu jinsi ilivyoenda. Ikaenda juu kule kupita Phoenix na kuvuka ng'ambo moja kwa moja, hata Prescott na kuvuka milimani hata Pwani ya Magharibi, moja kwa moja hata… Walikuwa wakienda wapi? Kule juu mpaka Alaska, na inanguruma, ikielekea kule.

74 Na vituo vya uchunguzi wa angani na wengine wote kule Tucson wangali wanauliza, watafiti wa

sayansi wanajaribu kuchunguza ni nini. Ilikuwa juu sana ambamo hakuwezi kupata ukungu, umande, ama cho chote kule. "Ilisababishwa na nini? Iko wapi?" Wao wametatanishwa vile vile na ile duara ya mbinguni inayoning'inia kule juu mbinguni kama walivyokuwa wale mamajusi walipokuja wakiifuata nyota, wakisema, "Yuko wapi aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" Ilikuwa ni kitu gani? Mungu akitimiza Neno Lake, "Na nyota itatoka katika Yakobo."

75 Naye Mungu wa Mbinguni aliahidi wakati wa jioni utakuwa na Nuru za jioni. Miaka mitatu iliyopita siri hii ilikuwa ni unabii, "Ni wakati gani, Bwana?" Lakini sasa ni historia. Imepita. Ahadi imetimizwa. Ni saa ngapi, bwana, na mvuto huu ni nini? Mungu akitimiza Neno Lake! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Hebu na tuombe.

76 Mungu mpenzi, nimewashikilia watu kwa muda mrefu, muda mrefu zaidi kuliko nilivyokusudia. Ninaomba, Mungu, ya kwamba jambo fulani lilisemwa au kufanywa ambalo litawafanya watu kila mahali kufahamu. Na kwa kuona na kufahamu huenda wakaamini ya kwamba Wewe ndiwe Kristo wa kweli, na Maneno yanayothibitishwa ni thibitisho la Neno Lake kuwa kamilifu na linatimizwa katika majira Yake.

Sasa, Bwana Yesu, kutokana na Maneno Yako Mwenyewe, Wewe ulisema ya kwamba ulimwengu ungekuwa katika hali ya Sodoma. Tunajua jambo hilo, tunaweza kuliangalia. Nawe ulisema, katika siku hiyo, "Kama ilivyokuwa katika Sodoma." Kulikuwako na wajumbe watatu waliotumwa kwa ulimwengu wa Mataifa na Waebrania. Na mmoja wao, ambaye alikuwa ni Mungu Mwenyewe, Mwana wa Adamu, alijifunua Mwenyewe katika umbo la kibinadamu na kufanya muujiza, hivi kwamba alimwambia Ibrahimu yale Sara aliyokuwa akifanya nyuma Yake hemani.

Ulisema ingejirudia tena wakati ulimwengu wote wa Mataifa ungekuwa katika hali ya Sodoma. Nasi tuko hapa, Bwana. Utabiri ule mwingine ukithibitisha jambo lile lile, kuhusu kutumwa kwa Eliya katika siku za mwisho, ile Roho ya Eliya juu ya nchi, kuleta mioyo ya baba, ama "ya watoto iwaelekee baba zao." Nami ninaomba, Mungu, ya kwamba saa hii ambayo Wewe utathibitisha Neno Lako, ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tujalie, Baba. Wote ni Wako. Ninaomba ya kwamba utatujalia baraka hizi na kuthibitisha yale yaliyosemwa, kwa ajili ya Utukufu wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

77 Kunena neno, ni mwanadamu; kuthibitisha neno, ni Mungu. Kusema jambo fulani, ni jambo moja; Mungu kufanya jambo hilo, ni jambo lingine. Mungu hahitaji mfasiri ye yote; Yeye hujifasiria Mwenyewe.

Sasa tunajiandaa kuwa na mstari wa maombi, kuwaombea wagonjwa, Mungu akipenda. Nasi tunajua ya kwamba hakuna mtu, hakuna mwanamume, hakuna mwanamke, hakuna mwanadamu, hakuna malaika, anayeweza kukuponya, kwa kuwa Mungu tayari amefanya hivyo. Yeye alifanya maandalizi, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuupokea.

78 Hakuna mtu, hakuna malaika, hakuna kitu, hata Mungu Mwenyewe, anayeweza kukusamehe dhambi zako. Tayari imekwisha. Yesu alifanya hivyo Msalabani. Bali haitakufanikisha kitu, ama kukufaidi kitu, hata utakapoukubali. Mnaona?

Jambo pekee liwezalo kufanywa, ni agizo ambalo limetolewa na Mungu, kwa waamini kuwekea wagonjwa mikono. Hiyo imekuwa katika nyakati zote wamefanya hivyo, kupitia miamsho. Nao wameiita, "Mungu."

79 Ibrahimu aliona ishara nyingi. Lakini kulifikia wakati ambao Ibrahimu aliona ishara yake ya mwisho, kabla tu Sodoma haijachomwa, na hiyo ilikuwa Mungu akijidhihirisha Mwenyewe katika mfano wa mwanadamu. Unaamini jambo hilo? Je! Yesu alisema ingejirudia?

80 Sasa, ni wangapi hapa … Na huko nje kwenye redio, ama huko kwenye simu kote nchini, kama bado ungali unasikiliza, jiandae sasa kwa ajili ya maombi, uwe unaomba, na ninyi mlio na leso hizi hapa. Sasa, siwezi kumwambia Mungu la kufanya. La. Jambo hili na liwe mbali nami hata kujaribu. Yeye ni mwenyezi; Yeye hufanya yale anayotaka. Ninaweza tu kutii na ninaweza tu kusema yale anayosema.

81 Na sasa wanasimama kote kutani, wamejaa, wamesongamana. Nashangaa kama tungeweza kumwuliza Mungu juu ya maneno haya, "Ni mvuto gani huu?" Kama Mungu angetenda miongoni mwetu tena (huenda kukawa na wageni hapa), na kutenda miongoni mwetu na kuonyesha uso Wake uliobarikiwa miongoni mwetu, akaonyesha Roho Wake yupo hapa, akaonyesha ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hata kila mmoja wetu ( baada ya Jumbe hizi mbili zenye nguvu) apate kuamini kwamba ni kweli? Mngeweza kufanya hivyo? Vema.

82 Badala ya kuagiza mstari wa maombi basi, kuna joto, msongamano, kusimama kuegemea ukutani Nikitazama huku kuagiza mstari wangu wa maombi, hamngeweza kuufanya kwa kusimama pale. Je, ningeweza kuuagiza upande *huu*? Ninyi mlio wagonjwa, machela, kila kitu, mliolala, hamngaliweza kuufanya. Kwa hiyo keti mahali ulipo, na umwamini Mungu. Kama una kadi ya maombi, ishikilie, itakuwa nzuri. Tutakufikia kama unataka kupitia kwenye mstari. Lakini si lazima upitie mstari.

83 Yule Bw. Shepherd, Jumapili iliyopita usiku, hakupitia kwenye mstari wo wote. Si—sidhani alikuwa na kadi ya maombi. Je! Bw. Shepherd yupo hapa usiku wa leo? Yuko wapi? Je! Yuko hapa? Yuko nyuma. Je! Ulikuwa na kadi ya maombi, Bw. Shepherd? Hukuwa nayo? Yeye hakuwa nayo. Yeye ameketi pale pale tena, usiku wa leo. Hapo ndipo mahali pazuri pa kuwa, Ndugu Shepherd.

84 Si kwamba inakupasa tu kuwa pale, bali uwe tu na imani. Kwa maana, kumbukeni, maskini mwanamke mmoja aligusa vasi Lake Naye akahisi huo. Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na waraka wa Waebrania, katika Agano Jipya, ulisema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu usiku wa leo anayeweza "kuchukuliana nawe katika mambo yako ya udhaifu." Unaamini jambo hilo? Iweni na imani basi! Msilitilie shaka. Aminini, na itatendeka. Mnaweza kupata yale—yale ambayo mmeomba, kama mnaweza kuiamini. Bali hauna budi kuamini. Utafanya hivyo? Je, ninyi nyote mtaamini jambo Hilo? Ni wangapi wataamini sasa? Mungu akubariki.

Sijui nani ni nani. Sijui hata mmoja wenu. Si kazi yangu kumjua ye yote wenu. Ni kazi ya Mungu kujua mambo haya. Lakini Yeye atafanya hivyo kama mtaamini. Utaamini sasa?

85 Sasa, Mungu Mpendwa, hakika sisi si kundi la Wakristo chotara, hatupaswi kuwa, mtu ambaye atabembelezwa na kubembelezwa. Wewe huna watu wa aina hiyo, Bwana. Una waamini waliokomaa. Uwepo halisi wa Mungu huwasha moto moyoni mwa mtu. Kama vile Ibrahimu, alivyomwamini Mungu. Ulijitambulisha kwake, ndipo ukamtokea na kufanya ishara, naye akakuamini. Uliugeuza mwili wake ukawa kijana mwanamume, na pia mkewe, ambaye, mkewe alikuwa sehemu ya mwili wake mwenyewe. Ndipo akaja yule mtoto mpya, yule mwana aliyeahidiwa.

86 Mungu, Wewe uliahidi ya kwamba lingekuwa ni jambo lile lile katika siku hii. Ninaomba ya kwamba utathibitisha Neno hili. Nasi tutashughulikia moja kwa moja juu ya hiyo ahadi moja pale, ya kwamba itakuwa kama ilivyokuwa huko Sodoma, kabla tu Sodoma haijateketezwa na hukumu kuikumba Sodoma, ulimwengu wa Mataifa. Kwa hivyo hukumu inakaribia kuupiga ulimwengu wa Mataifa, nao Wayahudi wana miaka mitatu na nusu zaidi kupitia wakati wa Dhiki, taabu yake Yakobo, kuendelea kwa majuma sabini ya Danieli. Bali majira ya Mataifa yamehesabiwa, ni wakati wa kuondoka. Nawe ulitoa ishara hiyo, na ukasema ya kwamba itakuweko tena. Tujalie, Mungu. Wao wako, tuko mikononi Mwako, tufanyie kama utakavyoona inafaa. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

87 Sasa msiwe na wasiwasi. Ingekuwaje kama nilikuwa na wasiwasi? Sasa, ninafanya jambo hapa ambalo halina budi kutegemea mamlaka ya Mungu. Lakini kwa nini nifanye hivi? Yeye alisema ingekuwa. Hilo latosha. Na kama akijithibitisha Mwenyewe hivyo mbele zenu, vema, hamuwezi kumwamini? Hakika. Iweni tu na imani sasa na mwamini.

Na hebu nitazame huku na huko, nikaone ambapo Roho Mtakatifu ataongoza, yale atakayotenda. Sijui atafanya nini, hiyo ni juu Yake. Lakini kama tu utakuwa na imani, amini tu, "Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio." Je, ninyi nyote mnaamini jambo hilo, inueni mikono yenu na kusema, "Ninaamini jambo Hilo." [Kusanyiko linasema, "Ninaamini jambo Hilo." — Mh.] Kwa moyo wangu wote, ninaamini jambo Hilo.

88 Basi, tatu itakuwa thibitisho, iwapo ataifanya mara tatu moja kwa moja kuwathibitishieni ya kwamba ni kweli. Sijali uko wapi, wewe ni nani, uwe tu na imani na ukaamini. Sasa, msi—msisogee. Upande *huu*.

Bibi, unayeomba, sikujui. Keti tu mahali ulipo; si lazima uje. Sikujui, bali umemshika msichana mdogo mkononi mwako, ama pajani mwako. Mimi ni mgeni kabisa kwenu. Na msichana huyo mdogo anaonekana wa kawaida, anaonekana mzima. Yeye ni msichana mdogo mrembo, msichana mdogo mwenye nywele nyekundu. Ninamwangalia hapa, yeye haonekani kana kwamba amelemaa ama cho chote kile. Sijui ana shida gani. Huenda isiwe ni kwa ajili ya mtoto huyo; huenda ikawa ni kwa ajili yako. Lakini ilitokea tu kukuona umeketi pale pamoja na mtoto huyo, na ukiomba. Inanibidi kunena nawe kwa muda mdogo kusudi nipate roho yako, kama Yesu alivyomwambia yule mwanamke, "Nipe maji ninywe," mnaona, kumchukua tu—kumfahamu tu mtu mmoja. Ndugu Bryant na hao wengine wanaoketi hapa, ninawajua watu hawa wanaoketi hapa. Huenda wakawa wahitaji, pia, bali ulikuwa mgeni.

Unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu? Je! Unaamini mambo haya ambayo umesikia usiku wa leo kuwa ni Kweli? Sasa, kama Mungu atanifunulia jambo fulani ambalo umefanya, ama jambo fulani ambalo hukupaswa kufanya, ama una kasoro fulani kwako, ama shauku yako ni nini, utajua kama ni kweli ama si kweli. Sivyo? Na iwapo atafanya hivyo, je, itathibitisha Neno Lake ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na ya kwamba Luka Mt. 17:30 tayari inadhihirishwa? Unaamini jambo Hilo?

89 Sasa, mama huyo aliinua mkono wake ya kwamba sisi ni wageni. Sikujui, bali ninajaribu kuwasiliana na roho yake, mtu mmoja. Kuna wengi wenu mnaovuta. Sasa, amini Haya kwa moyo wako wote.

Sasa, ni kwa ajili ya msichana huyo mdogo. Si wewe. Una wasiwasi, bali si wasiwasi unaokusumbua. Jambo kuu moyoni mwako ni yule msichana mdogo. Na unaamini Mungu anaweza kuniambia ni nini? Unaamini jambo hilo? Je! Ingekusaidia, ungeamini basi? Ni jeraha la ubongo. Hiyo ni kweli? Sasa weka

mkono wako juu ya kichwa cha mtoto huyo mdogo; mkono wako.

90 Mungu mpenzi, Wewe ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Mwanamke huyo ni mwaminio. Mkono wake uko juu ya mtoto huyo. Jalia apone. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba maombi haya. Amina.

Sasa mnaamini, ninyi nyote? Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana. Hakika!

Namjua bibi anayeketi karibu naye, bali anaangalia upande huu kwa unyofu sana. Siwezi kulitaja jina lake, bali mimi … Kama nikimwangalia kwa dakika moja, ningejua. Lakini ninamjua mwanamke huyo kwa sura, bali sijui shida yako ni nini. Je! Unaamini mimi … Mungu atanijulisha shida yako ni nini? Ungeweza … Ingekusaidia? Ugonjwa sukari. Sasa, kama hiyo ni kweli, shika mkono wako. Hakika!

Imetokea kuwa yule mama anayelala … anayeketi karibu nawe, ana jambo lile lile. Yeye ni mgeni. Yule mama mwingine anamwombea mtu fulani, mtoto kiwete. Amini kwa moyo wako wote, Mungu angemjalia.

91 Mtu fulani hapa nyuma. Mtu yule anayeketi kule anajaribu kuacha kuvuta sigara. Unaamini Mungu ataziondoa kwako? Vema. Unaamini? Unaweza kupokea. Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu.

Huyu hapa mtu. Je, mnaona lile wingu jeusi linalonig'inia juu ya mtu huyu papa hapa ambaye amelala katika kitu kama machela, au kiti? Yeye anakufa. Yeye ametiwa uvuli. Yeye ana kansa. Simjui mtu huyo, sijapata kumwona. Mungu anajua yote kukuhusu. Hiyo ni kweli, bwana. Unaamini Mungu angeweza kuniambia jambo fulani kukuhusu? Ingekusaidia kupokea uponyaji wako? [Ndugu huyo anasema, "Naam, ninaamini." — Mh.] Ulileltwa hapa na rafiki. Lakini wewe hutoki hapa, uko mahali fulani ambapo kuna maji mengi ambayo watu huvua samaki. ["Naam."] Naam, Albany, Kentucky. ["Hiyo ni kweli."] Hiyo ni kweli. Amini, nawe unaweza kurudi nyumbani, mzima. Amini ya kwamba imekwisha. Kama utaamini! Lazima uamini, na uamini ya kwamba imetendeka kwako. Unaamini?

92 Wewe, kutoka Tennessee, mna mvulana aliye na pumu. Si hapa, bali unaamini ya kwamba ataponywa? Basi mpelekee leso yako—mkononi mwako, kwenda kwake. Yeye ataponywa kama utaliamini Hilo.

Huyo mama analia, ameketi upande wa pili kutoka kwa Daktari Vayle pale. Yeye ametiwa uvuli, pia, kivuli cheusi. Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, bali ana kansa. Atakufa kama hajatendewa jambo fulani. Je! Unaamini atakuponya, bibi? Unaweza? Unaweza kupata uponyaji wako, kama utaamini tu.

Kuna bibi mdogo anayeketi moja kwa moja nyuma yake amevaa leso juu ya kinywa chake. Yeye pia ana tumbo lenye vidonda, mgonjwa. Umekuwa ukizirai, kupofuka, kuzimia. Mtu fulani alikuleta hapa. Una shida ya kike. Kama utaamini, unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima.

93 Wewe, kijana, ni mgeni, unayeketi papa hapa mbele zangu, ukinitazama. Wewe ni nani, M-Puerto Rico au nini? Naam, kile nilichomaanisha, …?…! Mimi ni mgeni kwako. Mnajua jambo hilo; hata hutoki nchini mwangu. Lakini unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukupa shauku ya moyo wako? Kama nitawaambia shauku yenu ni nini, mtalipokea? Unatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Mpokee Roho Mtakatifu, ndugu yangu.

Huyu hapa mtu mweusi ameketi nyuma kabisa hapa, ana mzigo moyoni mwake. Ni kwa ajili ya mke wake. Yeye hayupo hapa, hata. Ana shida ya miguu yake. Unaamini ya kwamba Yeye atamponya? Unaamini? Wewe ni mgeni hapa. Unatoka ng'ambo ya bahari. Umetoka Jamaica. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bw.Brady. Unaamini? Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

94 Bibi huyu anayeketi moja kwa moja upande huu, karibu na Bibi Wright pale, ana mzigo moyoni mwake. Yeye anamwombea binti. Yuko kwenye upasuaji. Unaamini kwa moyo wako wote, kwa ajili yake? Yeye hatauhitaji kama utamfanya kuamini. Siwezi kuponya.

Kule nyuma kabisa kwenye chumba cha watoto, namwona Roho Mtakatifu wa Mungu, ama Malaika, Nuru inayotulia katika chumba cha watoto. Imetulia juu ya kijana mwanamke, naye ana shida ya rohoni ambayo inamsumbua. Inaonekana kana kwamba ninapaswa kumjua mwanamke huyo, kwa namna fulani, msichana. Yeye pia ana ugonjwa wa kike. Ndiyo. Jina lake ni Bibi West, kutoka Alabama, Bibi David West. Amini; Mungu atakujalia.

95 "Kutakuweko Nuru, na siku ile anapofunuliwa Mwana wa Adamu." Kama huyo si Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, sijui kitu juu Yake. Unaamini Hilo? Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.

Kule nje kwenye vipaza sauti nchini mwote sasa, na katika Maskani haya, wangapi wenu watainua mikono yenu na kusema, "Mimi ni mwamini"? Sasa, ninyi huko nje katika nchi, kila mtu aliyeinua mikono yake juu, hapa. Na nje kule mbali sana mahali fulani nchini kote, mlioinua mikono yenu, bila shaka. Sasa funga macho yako, weka tu mikono yako juu ya mtu aliye karibu nawe. Shika mkono wake. Uwekelee

mbegani mwake. Nimeweka mikono yangu juu ya leso. Angalia yale yamefanywa leo! Angalia yale yaliyofanywa sasa.

Kuutazama uso Wake mbarikiwa
Unang'aa kwa upendo wa Kiungu;
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Kama vito katika taji Yake kung'aa.

Sasa ombeni. Hebu na tuombe, kila mahali.

96 Mungu mpenzi, wakati umewadia. Nini maana ya jambo hili? Mungu akitimiza Neno Lake! Kuna mvuto gani, Bwana? Ni Mungu akitimiza Neno Lake. Ni nini hii kote nchini, kupitia njia ya simu, ambapo mamia ya watu wamewekeana mikono kote nchini, kutoka pwani moja hadi nyingine, kutoka Kaskazini hadi Kusini, Mashariki hadi Magharibi? Hapa wameketi watu kutoka nchi za kigeni, wengi wa majimbo, Mexico, Canada, nasi tumewekeana mikono. Mungu akitimiza Neno Lake!

Inawezekanaje kwamba mtu anaweza kusimama hapa kwa Roho Mtakatifu na kumtambua mtu kama alivyomfanyia Simoni Petro, "Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona"?

"Nenda kamlete mumeo uje naye hapa."

"Sina mume."

"Hakika. Una watano."

Akasema, "Ninajua ya kwamba Masihi yuaja kufanya jambo hili, lakini Wewe ni Nani?"

Yeye alisema, "Mimi Ndiye."

97 Nawe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nawe umeahidi, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Zaidi ya haya mtafanya, kwa sababu mimi naenda kwa Baba." Na, tazama, siku za mwisho nitawapelekeeni Eliya, nabii, naye atabadilisha mawazo ya watu, ageuze mioyo ya watoto ielekee Mafundisho ya mitume ya Biblia. "Na itakuwa Nuru wakati wa jioni."

Tuko hapa, Mungu mkuu wa Mbinguni! Saa imewadia! Mikono iko juu ya watu.

Shetani, umeshindwa. Wewe ni mwongo. Na, kama mtumishi wa Mungu, na kama watumishi, tunakuamuru ya kwamba katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba utii Neno la Mungu na utoke ndani ya watu, kwa maana imeandikwa, "Katika Jina Langu watatoa pepo."

Na watu wote wapate kuwekwa huru. Tujalie, Mungu mpenzi. Wewe ndiye Mungu wa Mbinguni uliyeshinda, siku hiyo kwa mvuto juu ya Mlima Kalvari, magonjwa yote na maradhi na kazi zote za Ibilisi. Wewe ni Mungu. Nao watu wameponywa kwa mapigo Yako. Wao ni huru. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

98 Mungu, kila leso iliyo hapa, wakati Roho wa Mungu yuko, wakati upako wa Yesu Kristo umo juu ya watu, na ishara zile kuu alizoahidi tayari zinatimizwa, na dunia inatetemeka, matetemeko ya nchi yanatokea, zile ishara kuu alizosema, na Maandiko yanatimizwa, na Nuru ya jioni inamulika. Nalalia hizi leso kwa mwili wangu nikiwakilisha mwili huu wote wa waamini kutoka Mashariki, Magharibi, Kaskazini, na Kusini, na kumwambia Ibilisi, "Katika Jina la Yesu Kristo, mwache kila mgonjwa atakayewekelewa hizi," kwa ajili ya heshima na utukufu wa Neno la Mungu. Katika Jina la Neno la Mungu, Yesu Kristo wa Nazareti. Amina.

99 Sasa, kwa utulivu, busara, kiasi, na kwa uangalifu, kama waamini, je, sasa mnaamini na kukubali uponyaji wenu kutoka kwa Mungu Mwenyezi, katika Jina la Yesu Kristo? Kama mnaamini, inueni mikono yenu. Wote huko nje katika nchi, inueni mikono yenu huko nje. Kila mtu humu ndani, kadiri niwezavyo kuona, walikuwa wameinua mikono yao juu; ndani, nje, dhidi ya madirisha, milangoni, kwenye vitalu, na kote kila mahali, watu wameinua mikono yao. Wanakubali. Shetani ameshindwa! Mapigo ya Yesu Kristo yanakuponya, na Uwepo wa Yesu Kristo unathibitisha ukweli kwamba Yeye yu hai leo, anaweza daima kutimiza kila ahadi aliyofanya. Amina! Ninamwamini. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

100 Sasa hebu na tusimame kwa miguu yetu. Katika Jina la Bwana Yesu, tukikubali kila kitu ambacho kimefanywa au kusemwa, tunampenda kwa mioyo yetu yote. Tunamthamini kwa yote yaliyo ndani yetu. Sasa mnapoenda kwenye nyumba zenu mbalimbali tangu usiku wa leo, Mungu aambatane nanyi. Mungu akupe Roho Mtakatifu kama huna Roho Mtakatifu.

101 Kila mtu, mwanamke, mvulana, ama msichana, hapa, ambaye hajabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kuna nguo, bwawa. Usiahirishe mpaka kesho kile kinachoweza kufanywa leo. Huenda kesho ikawa imechelewa sana. "Yatosha kwa siku, maovu yake." Kuna wahudumu wamesimama, wanangojea, nguo zinangojea. Hakuna udhuru. Mnangoja? Kama uko hivyo, unaamini. Haidhuru namna gani umebatizwa, kunyunyiziwa, kumwagiwa, chochote kile, ni kosa. Nuru imekuja. Njoni, aminini, mkabatizwe.

Kila mtu asiye na Roho Mtakatifu, jalia umpokee Roho Mtakatifu, kila mmoja wenu, katika nguvu zote za Kiungu na upendo aliokuahidi, kukufanya kiumbe kipya ndani Yake. Mungu akubariki.

102 Sasa, mpaka Jumapili ijayo asubuhi saa tatu na nusu, hebu na tuimbe wimbo huu mdogo ambao tulikuwa tukiimba miaka mingi iliyopita.

Usisahau maombi ya familia,
Yesu anataka kukutana nawe kule;
Atakushughulikia na masumbufu yenu yote,
Msisahau maombi ya familia.

Hebu na tuuimbe huo pamoja sasa.

Msisahau maombi ya familia,
Yesu anataka kukutana nanyi hapo;
Atakushughulikia masumbufu yenu yote,
Loo, msisahau maombi ya familia.

Sasa tunapouimba huo tena, peaneni mikono na msafiri aliye karibu nawe, mnaona, tunapouimba.

Msisahau maombi ya familia,
Loo, Yesu anataka kukutana nanyi hapo;
Atakushughulikia masumbufu yenu yote,
Loo, msisahau maombi ya familia.

103 Hivi hamumpendi? Nampenda. Nampenda kwa sababu alinipenda kwanza na kununua wokovu wangu (huo ulikuwa ndio mvuto) juu ya Mlima Kalvari. Mvuto ule ule kwenye Mlima Sunset, Mlima Nebo, Mlima Sinai, matukio yote mbalimbali ya vilele vya mlima. Halafu, vema, hebu na tuuimbe sasa.

Nampenda, nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na ku- … wokovu
Mtini Kalvari.

Wote wampendao, waseme, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Na iwe hivyo! Sasa hebu wazia tu yale aliyokutendea; nadhani, ya kwamba ungeweza kuwa huko nje kwenye baa usiku huu. Labda mngekuwa kaburini kama vile nilipaswa kuwa, nje ya rehema za Mungu. Yeye alikufanyia nini? Loo, tungewezaje kujizuia tusimpende? Haileti tofauti yoyote yale mtu ye yote asemayo, Yeye ndiye wa kwanza.

104 Hebu na tufunge macho yetu, na tuinamishe vichwa vyetu tunapomwimbia Yeye sasa. Yeye anapenda nyimbo, kuimba nyimbo. Hebu na tumwimbie sasa.

Nampenda, nampenda
Sababu alinipenda (Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza)
Na kununua wokovu wangu
Mtini kwa Kalvari.

Huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa Mbele Zake, shukrani kwa yale macho yetu yameona, yale masikio yetu yameyasikia, yale yaliyoandikwa katika Neno la Mungu, yale ahadi Yake imekuwa kwetu leo. Mungu akubariki.

105 Tuna m—mgeni pamoja nasi usiku wa leo, ndugu, Ned Iverson, aliyekuwa mhudumu wa Kipresbiteri. Baba yake, ndugu zake, ni mhudumu wa Kipresbiteri. Yeye, ninaelewa, alibatizwa leo, tena, katika Jina la Yesu Kristo. Yeye ni mhudumu, na ni mzuri kwa hilo. Na sasa nitamuomba, kwa maana naamini ya kwamba yeye ni mtumishi wa Mungu, kuomba baraka za Mungu juu ya kusanyiko hili mnapoenda nyumbani.

Ndugu Iverson, njoo huku, huku tumeinamisha vichwa vyetu katika maombi. Mungu akubariki, ndugu yangu.

MESSAGE hub online

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7

www.messagehub.info